# UTEKELEZAJI

## WA ILANI YA UCHAGUZI OCTOBA 2015 HADI JUNE 2020

## JIMBO LA ILEMELA
MKOA WA MWANZA

**BAADHI YA MIRADI ILIYOFANYIKA KATIKA UONGOZI WA RAIS MAGUFULI**



Dr. John Pombe Joseph Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano
wa Tanzania




Ndege 11 Zilizotuwa



Daraja la Kigamboni



Train ya Umeme



Ubungo Interchange

**BAADHI YA MIRADI ILIYOTEKELEZWA KATIKA JIMBO LA ILEMELA**




MH. DKT. ANGELINE S.L MABULA (MB)
MBUNGE WA ILEMELA




Ferry Mv Illemela



Kituo cha Magonjwa ya mulipuko Buswelu



Barabara Sabasaba Kiseke- Buswelu



Tanki la Maji Kitangiri

**Tuliahidi, Tumetekeleza / Mshikamano wetu Ushindi wetu**

# TANZANIA MPYA CCM MPYA



***"TUNACHOHITAJI NI KUBADILIKA NA KUFANYA KAZI KWA BIDII. NA HII NDIO SABABU, TANGU KUINGIA MADARAKANI, SERIKALI YA AWAMU YA TANO IMEELEKEZA NGUVU NYINGI KATIKA KUREJESHA NIDHAMU YA WATUMISHI WA UMMA, AMBAO BAADHI YAO WALIJISAHAU NA HIVYO KUFANYA KAZI KWA MAZOEA."***

*Dr. John Pombe Joseph Magufuli,*
*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2017*

Yaliyomo


1.0 Utangulizi ........ 4
1.1 Ukubwa Wa Eneo Na Mgawanyo Wa Maeneo Ya Utawala ........ 5
1.2. Idadi Ya Watu ........ 6
2.0 Utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi 2015 – 2020 ........ 6
2.1 Utekelezaji wa ahadi za Mhe Rais, Makamu wa Rais na Mbunge ........ 7
2.2 Utekelezaji Wa Ilani Ya Uchaguzi Ya Chama Cha Mapinduzi Katika Sekta Mbalimbali ........ 47
2.3 Hali ya Uchumi ........ 7
3.0 Utekelezaji Wa Shughuli Katika Sekta Mbalimbali ........ 7
3.1 Sekta ya Raslimali Fedha ........ 7
3.1.1 Mwenendo wa mapokezi ya Ruzuku ya Serikali Kuu ........ 7
3.1.2 Mapato ya ndani ........ 7
3.2 Sekta ya Elimu ........ 8
3.2.1 Elimu ya Msingi ........ 8
3.2.2 Hali ya Miundombinu katika Shule za msingi ........ 9
3.2.3 Mapokezi ya Fedha za ruzuku ya elimu bila malipo ........ 10
3.2.4 Uandikishaji Darasa la awali mwaka 2020 ........ 10
3.3 Elimu ya Sekondari ........ 11
3.3.1 mapokezi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 ........ 14
3.3.2 HALI YA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE ZA SEKONDARI KWA MWAKA 2020 IKILINGANISHWA NA MWAKA 2015 ........ 14
3.3.3 Program ya EP4R ........ 15
3.3.4 Ukamilishaji wa Miundombinu katika shule ya Sekondari Buswelu ........ 15
3.4 Sekta ya Afya ........ 16
3.4.1 Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ........ 17
3.4.2 Kituo cha Afya Karume ........ 18
3.4.3 Kituo cha Afya Buzuruga ........ 19
3.4.4 Upatikanaji wa Dawa muhimu ........ 20
3.4.5 Uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na Saratani ya matiti ........ 20
3.4.6 Mapambano dhidi ya Malaria ........ 20
3.4.7 Huduma kwa Wazee na watu wenye Ulemavu ........ 21
3.5 Sekta ya Ardhi na Mipango Miji ........ 22
3.5.1 Urasimishaji Makazi ........ 22
3.5.2 Miradi ya Upimaji wa Viwanja ........ 22
3.5.3 Migogoro ya Ardhi ........ 23
3.5.4 Ukusanyaji wa kodi ya Ardhi ........ 25
3.6 Sekta ya Maji ........ 25
3.7 Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi ........ 30
3.7.1 Mikopo ya wanawake na vijana ........ 30
3.7.2 Uanzishwaji wa jukwaa la wanawake ........ 32
3.7.3 Uwezeshaji kiuchumi kaya masikini ........ 32
3.8 Mpango wa uboreshaji wa Makazi ........ 32
3.9 Sekta ya Viwanda ........ 32
3.10 Sekta ya Barabara ........ 33
3.11 Sekta ya Utawala na Raslimali Watu ........ 42
4.0 Changamoto zinazoikabili Wilaya ........ 50
6.0 Ujenzi wa chama na jumuiya zake ........ 52
7.0 Michango Ya Mbunge Kuimarisha Chama Na Jumuiya Zake ........ 57
8.0 Taasisi ya angeline foundation na uwezeshaji wa jamii ........ 59
9.0 Michango mbalimbali katika jamii ........ 62
10.0 Hamasa, michezo na utamaduni ........ 63
11.0 Ujenzi Wa Vituo Vya Michezo ........ 63
12.0 Ushiriki Wa Vikao ........ 66
13.0 Mahusiano Na Jamii ........ 68
14.0 Changamoto ........ 69
15.0 Shukurani ........ 69
16.0 Hitimisho ........ 70


## 1.0 UTANGULIZI

Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema kila iitwayo leo. Aidha niwashukuru wananchi wote wa Jimbo la Ilemela kwa ujumla wao na ushirikiano mkubwa ambao umeniwezesha kutenda kazi ya uwakilishi kwa ushirikiano mkubwa sana, tukiongozwa na kauli mbiu ya Jimbo **ILEMELA NI YETU, TUSHIRIKIANE KUIJENGA.** Hakika kauli mbiu hii imekuwa ni kichocheo kikubwa sana kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo kwa makundi yote; Wananchi, Viongozi, Wawakilishi,Viongozi wa Dini, Viongozi wa chana na hata Serikali pia. Ushirikiano umekuwa mkubwa sana kwa kipindi chote.

Aidha namshukuru sana Mhe Dkt John P.J.Magufuli Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini kuwa msaidizi wake katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kipindi chote tangu Serikali ya awamu ya tano iingie madarakani, nasema asante sana, name nakuahidi kuwa katu sitakuangusha.

Taarifa hii ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2015 – 2020, ni mwendelezo wa taarifa ambazo nimekuwa niitoa mara kwa mara kuonesha kazi zilizofanyika katika kipindi husika. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi umedhihirisha kuwa Serikali ya awamu ya tano imedhamiria kwa dhati na kujikita zaidi katika kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi ili kuboresha maisha yao na kuendeleza amani na mshikamano uliopo miongoni mwa wananchi. Aidha, dhamira ya Serikali ni kuleta maendeleo ya Kijamii, Kiuchumi na kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo Mwaka 2025, kupitia sekta ya viwanda. Mbali na mambo mengine, Serikali imekuwa ikisisitiza ushirikishwaji wananchi kufanya kazi na kumtaka kila mmoja wetu kuwa mzalendo kwa nchi yake huku ikihimiza uwekezaji kwenye viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa kama mambo ya msingi ili kufanikisha dhamira ya kuufikia uchumi wa kati ifikapo 2025.

Kwa ufupi, taarifa hii imeeleza mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji shughuli mbalimbali za kisekta chini ya Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi(CCM).



### 1.1 UKUBWA WA ENEO NA MGAWANYO WA MAENEO YA UTAWALA

Jimbo la Ilemela lina ukubwa wa square mita za mraba 1,080.55 kati ya hizo eneo la maji ni kilomita za mraba 828.45 nchi kilomita  za mraba 252.10 Tarafa 1 Kata 19, Mitaa 171, Matawi ya Chama 126, Jimbo moja la uchaguzi lililo chini ya CCM na Mbuge wake ni Dkt. Angeline S. L.Mabula (Mb)



**Picha ya pamoja kuanzia Kushoto Ndg Kadio aliyekuwa RAS mwanza kwasasa ni Katibu Mkuu wizara ya mambo ya ndani, RC Mhe John Mongela, Mbunge wa Ilemela Dr Angeline Mabula  na RAS mpya Ndg Tutuba**



**Baadhi ya wenyeviti wa Serikali za Mitaa wakila kiapo mara baada ya kutangazwa washindi katika uchaguz uliofanyika mwaka 2019**

## 1.2 IDADI YA WATU

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya wata na makazi mwaka 2012, Wilaya ilikuwa na watu takribani 343,001 kati ya hao Wanaume ni 164,718 na Wanawake ni 178,283. Aidha kwa sasa inakadiriwa kuwa na watu 475,774 kati ya hao wanaume ni 220,976 na wanawake ni 236,798 kwa makadrio ya mwaka 2019.

## 2.0 Utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi 2015 – 2020

Ilani cha CCM ya mwaka 2015 – 2020 imeandikwa kwa kuzingatia mambo makuu yafuatayo;

- Kuendelea kushika dola kwa kuwaongoza watanzania kwa njia ya kidemokrasia.
- Utekelezaji wa Ilani kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, na mwelekeo wa Sera za CCM zenye lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi.
- Kuondoa umaskini wa kipato.
- Kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira.
- Kuendeleza vita dhidi ya adui rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.
- Kuendelea kudumisha Amani, Ulinzi na Usalama wa maisha ya wananchi na mali zao.

## 2.1 Utekelezaji wa ahadi za Mhe Rais, Makamu wa Rais na Mbunge

Ni jambo la kumshukuru mungu sana kwa kipindi cha miaka 5 ya mwanzo ya awamu ya tano chini ya uongozi wa Jemedari wetu Dkt John P.J. Magufuli akisaidiwa na Makamu wa Rais Mama Samia Suhuhu Hassan na Waziri Mkuu Mhe Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa Jimbo la Ilemela ahadi zote zilizotolewa zimetekelezwa kwa asilimia 99.9. Hii inajidhihirisha wazi kuwa kazi kubwa zilizofanyika kama zitakavyoonekana katika taarifa hii. Ahadi zilizotekelezwa:

1. Uboreshaji Miundombinu ya Elimu ya Msingi na Sekondari ili kuweka mazingira mazuri ya kufundisha na kujifunzia.
2. Uboreshaji Mazingira katika vituo vya afya na zahanati na kuongeza ama kuanzisha nyingine mpya.
3. Uanzishwaji mashindano ya Jimbo Cup ili kuibua vipaji kwa vijana.
4. Kusogeza huduma ya maji hasa katika maeneo yenye shida kubwa ya maji kwa kushirikiana na mamlaka ya maji MWAUWASA, Manispaa ya Ilemela na wadau mbalimbali.
5. Uboreshaji miundo mbinu ya Barabara ikiwemo kufufua barabara zilizokuwa zikitumika enzi za ukoloni.
6. Kutoa elimu ya ujasiliamali kwa wanawake, Vijana na Mabalozi.
7. Kusimamia kwa karibu kutengwa 10% ya kila mwezi katika mapato ya ndani ya Halmashauri na kuwawezesha vikundi mbalimbali kupata mikopo.
8. Uboreshaji mazingira ya wauza kahawa katika mitaa yetu.
9. Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi zote za Mhe Rais Dr. John Pombe Joseph Magufuli, na Makamu za Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan.
10. Kuboresha vituo vya Polisi ikiwemo ukamilishaji wa nyumba ya askari kata ya Kiseke na kituo cha Polisi Kata ya Ilemela kwa kushirikiana na Kata husika.
11. Kuweka umeme katika Jengo la kituo cha Polisi Kata ya Bugogwa.
12. Kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa waendesha bodaboda. Ahadi hii bado haijatekelezwa kutokana na Mamlaka ya upangaji miji utoanisha vituo vya bodaboda

**2.2 UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI KATIKA SEKTA MBALIMBALI**

Jimbo la Ilemela ambalo Mbunge ni mwakilishi wake, wakisaidiana kwa karibu sana na Uongozi mzuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa maana ya Baraza la Madiwani chini ya **Meya Renatus Mulunga,** Watendaji wote wakiongozwa na Wakili Msomi **Ndugu John Paul Wanga,** tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana, kutekeleza shughuli za maendeleo katika *Sekta za Elimu, Afya, Maji, Kilimo na Ushirika, Utawala, Ardhi na Mipango Miji, Mifugo na Uvuvi, Hifadhi ya Mazingira, Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi na Uwekezaji wa viwanda na Biashara* kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2015 - 2020 kama ifuatavyo;

**2.3 Hali ya Uchumi**

Sekta ya fedha ndio kipimo cha kuonesha kiwango cha uchumi wa nchi uliofikiwa, na uimara na uwezeshaji wa sekta hii huleta maendeleo ya haraka katika Taifa. Manispaa imesimamia utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi kwa mafanikio makubwa japokuwa si maeneo yote ambayo yamefanikiwa kufikia malengo.

Aidha ukusanyaji mapato unaendelea kusimamiwa kwa karibu kwa kuongeza udhibiti wa ukusanyaji mapato kwa kutumia njia ya kielektroniki. Ili kuongeza ufanisi na udhibiti wa upotevu wa mapato yanayokusanywa. Wilaya inatumia mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa kielektroniki ambapo hadi sasa ina mashine za kukusanyia mapato 185. Aidha, imefunga mfumo wa kukusanya mapato katika vituo vyote vya kutolea huduma za Afya vya Buzuruga, Karume na Sangabuye, baada ya kufunga vifaa hivyo mapato yameongezeka mara dufu.

**3.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KATIKA SEKTA MBALIMBALI**

Halmashauri imefanikiwa kutekeleza shughuli za maendeleo katika sekta za Rasilmali fedha, Elimu, Afya, Maji, Kilimo, Utawala, Ardhi na Mipango Miji, Mifugo na Uvuvi, Hifadhi ya Mazingira, uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi, viwanda na Biashara kama ifuatavyo**:-**

**3.1 Sekta ya Raslimali Fedha**

**3.1.1 mwenendo wa mapokezi ya Ruzuku ya Serikali Kuu**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, imeendelea kupokea Ruzuku ya fedha kutoka Serikali Kuu ambapo mapokezi yamekuwa kama jedwali linavyoonesha hapa chini**:-**

| Na | Mwaka | Makisio | Mapato | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2015/2016 | 51,084,236,731 | 39,521,571,065 | 77 |
| 2. | 2016/2017 | 49,488,727,421 | 42,140,676,111 | 85 |
| 3. | 2017/2018 | 45,754,219,486 | 37,152,254,665 | 81 |
| 4. | 2018/2019 | 64,331,406,234 | 37,130,556,924 | 81 |
| 5. | 2019/2020<br>(to April) | 59,185,411,023 | 37,421,811,673 | 63 |

**3.1.2 Mapato ya ndani**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, kwa kushirikiana na jamii imefanikiwa kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato kutoka **Tshs.6,550,009,000.00** Mwaka **2015/2016** makusanyo halisi yalikuwa **Tshs. 4,852,625,944.25** sawa na **asilimia 74,** ukilinganisha na bajeti ya **2019/2020 Tshs 8,878,387,000.00** na makusanyo halisi ha **April 30, 20202 ni Tshs. 8,131,783,383.00** sawa na **asilimia 92** ya makisio.

Mafanikio haya yanatokana na mwitikio mzuri wa jamii kulipa kodi na ushuru mbalimbali wa Serikali na pia mwamko katika kuchangia shughuli za maendeleo ya Wilaya haya yanajionesha kwenye jedwali lifuatalo:-

**3.1.3 Mwenendo wa ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri ilipoanzishwa hadi Machi mwaka wa fedha 2019/2020**

| Na | Mwaka | Makisio | Mapato halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2015/2016 | 6,550,009,000.00 | 4,852,625,944.25 | 74% |
| 2. | 2016/2017 | 6,524,495,000.00 | 5,530,177,997.00 | 85% |
| 3. | 2017/2018 | 11,753,610,000 | 4,649,865,748.93 | 40% |
| 4. | 2018/2019 | 9,024,065,000.00 | 8,051,895,514.00 | 89% |
| 5. | 2019/2020 (April,2020) | 8,878,387,000.00 | 8,131,783,383.00 | 92% |

## 3.2 Sekta ya Elimu

### 3.2.1 Elimu ya Msingi

Kutokana na tamko la Mhe Rais la kuwa na sera ya elimu bila malipo, utekelezaji wa Ilani umekuwa na changamoto kubwa hasa katika Miundombinu ya Vyumba vya Madarasa, Matundu ya vyoo, Madawati, Nyumba za Waalimu n.k. Kutokana na ongezeko kubwa la wanafunzi kushirikishwaji wa jamii ulipewa kipaumbele katika kuchangia ujenzi wa miundombinu. Wananchi waliitikia wito huo na matokeo chanya yalionekana wazi kwa kuwa na ongezeko kubwa la vyumba vya madarasa na uanzishwa wa shule 3 mpya za msingi ambazo ni: *Shule ya msingi Kayenze ndogo iliyopo kata ya Bugogwa, shule ya msingi Ihalalo Kata ya Sangabuye na Shule ya msingi Base Kata ya Kayenzi.*



Shule mpya ya Msingi IHALALO Kata ya SANGABUYE iliyojengwa kwa msaada wa marafiki toka Jiji la DEAGU nchini Korea ya Kusini.




Watoto wa shule ya Msingi Nyamwilikelwa iliyoko kata ya Mecco wakiwa wanafurahia madawati yaliyotolewa na taasisi ya Angeline Foundation

**Idadi ya shule za msingi mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2015**

| Na | Umiliki wa Shule | Mwaka 2015 | Mwaka 2020 | Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shule za Serikali | 72 | 75 | 3 |
| 2 | Shule Binafsi | 29 | 52 | 23 |
| | **Jumla** | **101** | **128** | **27** |

**Idadi ya wanafunzi shule za msingi Mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2015**

Jumla ya wanafunzi 7**5,551** kati yao wavulana ni **36,641** na wasichana ni **38,910** wamesajiliwa katika shule za msingi za Serikali. Vile vile, jumla ya wanafunzi **13,224** kati yao wavulana ni **6,656** na wasichana ni **6,568** wamesajiliwa katika shule za msingi za binafsi kama inavyoonesha kati jedwali hapa chini;

| Na | Umiliki wa Shule | 2015 | 2020 | Ongezeko | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Shule za Serikali | 64,229 | 75,551 | 11,322 | 17 |
| 2 | Shule Binafsi | 9,037 | 13,224 | 4,187 | 46 |
| | **Jumla** | **73,266** | **88,775** | **15,509** | **21** |

**3.2.2 Hali ya Miundombinu katika Shule za msingi**

Kwa kushirikisha jamii Serikali ya awamu ya tano imeendelea kuboresha na kujenga miundo mbinu mipya katika shule za msingi hivyo na hivyo kuongeza idadi ya miundombinu kwa kuongeza vyumba vya Madarasa **69**, Matundu ya vyoo **86**, Nyumba za walimu **4** pamoja na Madawati **7,605**. Miundombinu yote kwa kiasi kikubwa imejegwa kwa mfumo wa Utatu katika shughuli za Maendeleo, *yaani Wananchi, Ofisi ya Mbunge na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela* na mingine kuna mkono wa Serikali Kuu.

**Hali ya miundombinu katika Shule za msingi kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2015**

| Na | Aina ya Mradi | iliyokuwepo 2015 | iliyopo 2020 | Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Madarasa | 511 | 580 | 69 |
| 2 | Matundu ya Vyoo | 791 | 877 | 86 |
| 3 | Madawati | 12,476 | 20,081 | 7605 |
| 4 | Nyumba za walimu | 80 | 84 | 4 |

**Hali ya Upungufu wa Miundombinu Elimu Msingi kwa mwaka wa fedha 2019/2020**

Pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali pamoja na wananchi, bado Shule za msingi katika Manispaa ya Ilemela zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa Miundombinu na Samani ambapo hadi kufikia Machi 2020, kulikuwa na upungufu wa Madawati **11,351,** Matundu ya vyoo **2,705,** Nyumba za walimu **1,606** na vyumba vya Madarasa **1,268** kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapa chini**:-**

| NA | MAELEZO<br>Aina ya miundombinu | Mahitaji | Iliyopo | upungufu | % upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Vyumba vya madarasa | 1,848 | 580 | 1,268 | **67** |
| 2. | Matundu ya vyoo | 3,680 | 975 | 2705 | **74** |
| 3. | Madawati | 31,432 | 20,081 | 11,351 | **36** |
| 4. | Nyumba za walimu | 1,688 | 82 | 1,606 | **95** |

### 3.2.3 Mapokezi ya Fedha za ruzuku ya elimu bila malipo

Tunamshukuru sana Mhe Rais Dkt. J.P.J Magufuli kwa kuendelea kutoa fedha za ruzuku moja kwa moja kwenye shule zetu. Serikali ya awamu ya tano, kuanzia mwezi Desemba 2015 hadi February, 2020 Manispaa ya Ilemela kimeokea fedha ya ruzuku ya Elimu bila malipo katika shule zote 75 za msingi . Hadi sasa fedha zilizotolewa na kupokelewa ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Na | Mwaka | Lengo | Mapokezi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2015/2016 | 275,340,000.00 | 275,340,000.00 | 100 |
| 2. | 2016/2017 | 410,000,972.25 | 410,000,972.25 | 100 |
| 3. | 2017/2018 | 415,728,527.01 | 415,728,527.01 | 100 |
| 4. | 2018/2019 | 402,242,663.81 | 402,242,663.81 | 100 |
| 5. | 2019/2020 | 250,640,440.63 | 250,640,440.63 | 100 |
| **Jumla** | | **1,753,952,603.70** | **1,753,952,603.70** | **100** |

Fedha za posho ya madaraka kwa walimu wakuu zilianza kutolewa kuanzia Julai, 2017 ambapo hadi Machi, 2020 jumla ya **Tshs. 461,600,000.00** zimetolewa.

Fedha za chakula kwa wanafunzi hadi Machi, 2020 kiasi cha **Tshs. 220,743,601.48** zimetolewa na fedha za posho ya maafisa elimu kata kiasi cha **Tshs. 147,250,000.00** kimetolewa hadi Machi, 2020.

### 3.2.4 Uandikishaji Darasa la awali mwaka 2020

Kutokana na mwitikio chanya wa wananchi juu ya tamko la Mhe Rais la elimu bila malipo, uandikishaji watoto wa darasa la awali umekuwa kwa miaka yote mitano umevuka lengo lililokusudiwa. Hadi kuishia Machi 2020, Halmashauri iliweza kuandikisha watoto **6,098** sawa na **asilimia 86** ya lengo la kuandikisha watoto **7,109.** Aidha, Halmashauri kuanzia Mwaka **2015 hadi 2019** mara baada ya kuanzishwa kwa mpango wa elimu bila malipo, imefanikiwa kuvuka malengo ya uandikishaji kwa kila mwaka kama ilivyooneshwa kwenye jedwali hapo chini:-

| Mwaka | Lengo | Walioandikishwa | | | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wasichana | Wavulana | Jumla | |
| 2015 | 7382 | 4028 | 3832 | 7860 | 107 |
| 2016 | 7837 | 4571 | 4504 | 9075 | 169 |
| 2017 | 7667 | 4359 | 4291 | 8650 | 113 |
| 2018 | 7450 | 4010 | 4076 | 8,086 | 109 |
| 2019 | 7413 | 4070 | 4242 | 8312 | 112 |
| 2020 | 7109 | 3024 | 3074 | 6098 | 86 |
| | | | | | |

### 3.2.5 Uandikishaji Darasa la Kwanza mwaka 2020

Kama ilivyo katika uandikishaji wa darasa la awali, katika elimu ya msingi pia mafanikio yamekuwa makubwa sana. Kwa mwaka 2020 Manispaa ya Ilemela imefanikiwa kuandikisha wanafunzi **10,797** sawa na **asilimia 108** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **9,955.** Kufuatia Mpango wa Serikali wa elimu bila malipo kumekuwa na ongezeko kubwa la uandikishaji hivyo kusababisha changamoto ya upungufu wa miundombinu na samani kwa shule za Awali na Msingi. Pia, wanafunzi wengi wenye rika la kuanza shule wameweza kuandikishwa tofauti na miaka ya awali. Katika kipindi chote, Wilaya iliweza kuandikisha kwa zaidi ya **asilimia 110.5** ya lengo kama ilivyooneshwa katika jedwali hapa chini**:-**

| Mwaka | Lengo | Walioandikishwa | | | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wasichana | wavulana | Jumla | |
| 2015 | 7,950 | 4595 | 4396 | 8,991 | 112 |
| 2016 | 9,168 | 7598 | 7286 | 14,884 | 162 |
| 2017 | 11,716 | 6185 | 5953 | 12,138 | 103 |
| 2018 | 10,574 | 6278 | 5863 | 12,141 | 115 |
| 2019 | 10,440 | 5266 | 5845 | 11,532 | 110 |
| 2020 | 9,955 | 5488 | 5309 | 10797 | 108 |

**3.2.6 Hali ya ufaulu wa Mtihani wa Darasa la Saba**

Kwa miaka mitano mfululizo Halmashauri ya manispaa ya Ilemela imeendelea kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa na hibyo kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa katika shule kumi bora ka ufaulu wa wanafunzi wa darasa na saba. Ukiondoa mwaka 2017 ilikuwa nafasi ya 20. Kiwango cha ufaulu wa wanafunzi wa darasa la saba kimeongezeka kutoka asilimia 89.8 mwaka 2015 hadi asilimia 97.55 mwaka 2019. Ufaulu umekua wa juu ukilinganishwa na malengo ya BRN, kwa Manispaa ya Ilemela ufaulu ni zaidi ya aslimia 80 ya BRN kama inavyoonekana hapo chini.

| MWAKA | WALIOFANYA | | | WALIOFAULU | | | ASILIMIA YA UFAULU | NAFASI YA WILAYA KIMKOA | NAFASI YA WILAYA KITAIFA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JUMLA | | | |
| 2015 | 3353 | 3714 | 7067 | 3104 | 3210 | 6314 | 89.8 | 2 | 10 |
| 2016 | 3700 | 3850 | 7550 | 3506 | 3417 | 6923 | 91.7 | 2 | 9 |
| 2017 | 4681 | 5109 | 9790 | 4268 | 4301 | 8569 | 87.5 | 2 | 20 |
| 2018 | 4187 | 4695 | 8882 | 4055 | 4365 | 8420 | 94.80 | 1 | 6 |
| 2019 | 4269 | 4661 | 8930 | 4207 | 4504 | 8711 | 97.55 | 1 | 2 |

## 3.3 Elimu ya Sekondari

Katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015-2020, Halmashauri imefanikiwa kuanzisha shule mpya tatu za kidato cha kwanza hadi cha nne ambazo ni: *Shule ya Sekondari Kayenze Kata ya Kayenze, Angeline Mabula Kata ya Kiseke na Shule ya Sekondari ya Kisundi Kata ya Bugogwa.* Aidha uanzishwaji wa shule 2 za kidato cha tano na sita katika Shule ya Sekondari Buswelu natayari imeshapangiwa wanafunzi wapo shuleni tayari.

Aidha mchakato wa kuanzisha kidato cha tano na sita katika Shule ya sekondari Sangabuye unaendelea. Kwa sasa Manispaa ina shule za Sekondari 50 kati ya hizo shule 27 ni za Serikali na shule 23 ni za binafsi. Jumla ya wanafunzi **27,811** wamesajiliwa katika Shule za Sekondari za Serikali. Pia, Kwa mwaka **2018/2019** shule ya Sekondari Buswelu imeanzisha masomo ya Kidato cha tano kwa Michepuo ya PCB na PGM ambapo mpaka sasa wanafunzi wameripoti na wanaendelea na masomo.



Moja ya majengo ya shule mpya zilizojengwa kipindi hiki Shule ya Sekondari ya KAYENZE Kata ya Kayenze.



Majengo mapya ya Kidato cha Tano na cha Sita katika shule ya Sekondari ya Sangabuye.



Moja ya chumba cha maabara katika Sekondari ya Sangabuye kinavyoonekana kwa ndani.







Ofisi ya Waalimu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bwiru iliyofanyiwa ukarabati mkubwa na mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)




Bwalo la Chakula katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bwiru iliyofanyiwa ukarabati mkubwa na mamlaka ya Elimu Tanzania



Jengo la Hostel katika Shule ya kwa ajili ya Wasichana katika Shule ya Sekondari ya BUSWELU




Moja ya choo kilichofanyiwa ukarabati na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) katika Shule ya Sekondari ya wasichana ya Bwiru.



Moja ya vyumba vya kulala wanafunzi wa bweni katika Shule ya Sekondari ya Buswelu kama inavyoonekana baada ya samani zote kukamilika na kuwekwa vyumbani.

### 3.3.1 MAPOKEZI YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA KUANZIA MWAKA 2015 HADI 2020

Idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa kidato cha kwanza imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka toka asilimia 88% mwaka 2015 hadi asilimia 97% mwaka 2020. Jumla ya wanafunzi 8,529 wakiwepo wav 4,223 na was 4,306 wameripoti shuleni sawa na asilimia 97% ya wanafunzi 8808 (wav 4317 na was 4491) waliopangwa. Kati ya hawa wanafunzi 7697 (wav 3799 Was 3898) sawa na asilimia 79.83 ndio walioripoti shule za serikali na wanafunzi 832 (wav 424 was 408) sawa na asilimia 9% wameripoti shule za binafsi. Aidha asilimia 3.2% bado watendaji wa kata ma maafisa elimu kata wanaendelea wafuatilia ili kuthibitisha shule walizokwenda kuripoti kupitia kwa wazazi wao kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

**Hali ya Mapokezi Kidato cha kwanza mwaka 2015-2020**

| Mwaka | Lengo | Walioandikishwa | | | Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wasichana | Wavulana | Jumla | (%) |
| 2015 | 6,324 | 2914 | 2705 | 5,619 | 88 |
| 2016 | 6239 | 2748 | 2622 | 5,370 | 86 |
| 2017 | 6243 | 2765 | 3040 | 5,807 | 92 |
| 2018 | 8,420 | 3,860 | 4,365 | 8,225 | 97 |
| 2019 | 8,359 | 3,968 | 4,339 | 8,307 | 99 |
| 2020 | 8,808 | 4,223 | 4,306 | 8,529 | 97 |

### 3.3.2 Hali ya Miundombinu katika Shule za Sekondari kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na mwaka 2015

Idadi ya miundombinu imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka kwa jitihada mbalimbali inazofanywa na jamii, ofisi ya Mbunge, Halmashauri na serikali kuu. kama ifuatavyo:

| AINA | IDADI 2015 | IDADI 2020 | ONGEZEKO |
|---|---|---|---|
| Vyumba vya Maadarasa | 320 | 374 | 54 |
| Matundu ya Vyoo | 286 | 370 | 84 |
| Meza | 14726 | 18,366 | 3640 |
| Viti | 14726 | 18,366 | 3640 |
| Vyumba vya maabara | 59 | 72 | 13 |
| Nyumba za walimu | 86 | 87 | 1 |

Shule za Sekondari katika Wilaya bado zinakabiliwa na upungufu wa miundombinu na samani ambapo hadi kufikia Mwezi Juni, 2020, katika shule za sekondari tuna mahitaji ya vyumba vya madarasa 620 vilivyopo 374 na pungufu 246, mahitaji ya matundu ya vyoo 1121 yaliyopo 370 na pungufu 751, viti na meza 24,790 yaliyopo ni 18,478 na upungufu ni 6,282 vyuma vya maabara mahitaji ni 81 vilivyopo 66 na upungufu ni 15. Nyumba za walimu mahitaji ni 1016 zipo 87 na upungufu 929. Mahitaji yamekuwa yakiongezeka kutokana na ongezeko la uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka hadi mwaka na hivyo mahitaji ni kama inavyooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:-

**Mahitaji na upungufu wa miundombinu**

| Na. | Maelezo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Aina** | **Mahitaji** | **Iliyopo** | **Upungufu** | **Upungufu %** |
| 1 | Vyumba vya Maadarasa | 620 | 374 | 246 | 40 |
| 2 | Matundu ya Vyoo | 1121 | 370 | 751 | 67 |
| 3 | Meza | 24,790 | 18,366 | 6424 | 26 |
| 4 | Viti | 24,790 | 18,366 | 6424 | 26 |
| 5 | Vyumba vya maabara | 81 | 66 | 15 | 19 |
| **6** | **Nyumba za walimu** | 1016 | 87 | 929 | 91 |

### 3.3.3 Program ya EP4R

Kwa mwaka 2018/19 Halmashauri ilipokea fedha za EP4R ambapo Elimu sekondari ilipokea jumla ya Kiasi cha Tshs. **62,338,371.804** kwa ajili ya ukusanyaji wa takwimu na urekebishaji wa Ikama ya walimu 24. Pia, Halmashauri ilipokea kiasi cha fedha **Tshs. 232,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Bwalo, madarasa manne na chumba kimoja cha maabara. Kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi kufikia March 2020.

### 3.3.4 Ukamilishaji wa Miundombinu katika shule ya Sekondari Buswelu

Halmashauri katika kutekeleza maagizo ya Serikali ya kuwalinda watoto wa kike walioko shuleni, imejenga bweni la wasichana lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 96 katika shule ya sekondari Buswelu ambapo ujenzi umekamilika na limeanza kutumika.

### 3.3.5 Mapokezi ya Fedha za ruzuku ya Elimu bila malipo

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imepokea fedha kwa ajili ya elimu bila malipo kiasi cha Tshs. 7,471,872,790.18 kuanzia mwaka 2015 hadi kufikia February, 2020. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa unaoneshwa katika jedwali lifuatalo**:-**

| Na | Mwaka wa Fedha | Mapokezi |
|---|---|---|
| 1. | 2014/2015 | 129,786,000.00 |
| 2. | 2015/2016 | 1,634,868,000.00 |
| 3. | 2016/2017 | 1,664,165,376.00 |
| 4. | 2017/2018 | 1,613,443,584.00 |
| 5. | 2018/2019 | 1,543,306,144.00 |
| 6. | 2019/2020 | 886,303,686.18 |
| **JUMLA** | | **7,471,872,790.18** |

### 3.3.6 Hali ya mimba za wanafunzi mashuleni

Ili kukabiliana na changamoto ya mimba shuleni Halmashauri imeendesha zoezi la upimaji wa mimba kwa wanafunzi. Jumla ya wanafunzi 23 toka shule mbalimbali wamebainika kuwa na ujauzito na kesi zao zimewasilishwa katani na polisi kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za kisheria.

### 3.3.7 Hali ya ufaulu wa mtihani wa kidato cha nne

Hali ya ufaulu imeongezeka kutoka asilimia 85.22% kwaka 2016 hadi asilimia 87.66% kwa kidato cha nne mwaka 2019, kutoka asilimia 96.8% mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 99.34% mwaka 2019 kwa kidato cha sita kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:-

## MATOKEO KIDATO CHA PILI

| MWAKA | IDADI YA WATAHINIWA | MADARAJA | | | | | GPA | ASILIMIA (%) | NAFASI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | 0 | | | KIMKOA | KITAIFA |
| 2016 | 4689 | 252 | 752 | 972 | 1923 | 790 | 3.2531 | 96.81 | 1 | 12 |
| 2017 | 6462 | 1406 | 931 | 1201 | 2601 | 323 | 3.2937 | 94.79 | 1 | 15 |
| 2018 | 6871 | 1756 | 901 | 1078 | 2680 | 456 | 3.4415 | 93.36 | 1 | 19 |
| 2019 | 8118 | 1406 | 1036 | 1325 | 3852 | 499 | 3.4358 | 93.85 | 2 | 30 |

## MATOKEO KIDATO CHA NNE

| MWAKA | IDADI YA WATAHINIWA WALIOFANYA | WALIOFAULU | MADARAJA | | | | | GPA | ASILIMIA (%) | NAFASI | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | I | II | III | IV | 0 | | | KIMKOA | KITAIFA |
| 2016 | 4682 | 3935 | 248 | 806 | 990 | 1891 | 747 | 3.6468 | 85.22 | 1 | 6 |
| 2017 | 5278 | 4405 | 211 | 822 | 1098 | 2274 | 873 | 3.7116 | 83.46 | 2 | 19 |
| 2018 | 5106 | 4361 | 295 | 873 | 1087 | 2106 | 745 | 3.60054 | 85.41 | 1 | 17 |
| 2019 | 5647 | 4950 | 418 | 908 | 1243 | 2381 | 697 | 3.5888 | 87.66 | 2 | 17 |

### MATOKEO KIDATO CHA SITA

| MWAKA | IDADI YA WATAHINIWA | MADARAJA | | | | GPA | ASILIMIA (%) | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | 0 | | |
| 2016 | 1189 | 83 | 398 | 580 | 90 | 38 | 3.5649 | 96.8 |
| 2017 | 986 | 63 | 291 | 500 | 83 | 49 | 3.5122 | 96.13 |
| 2018 | 958 | 65 | 384 | 459 | 41 | 9 | 3.4036 | 99.06 |
| 2019 | 916 | 129 | 327 | 422 | 32 | 6 | 3.3677 | 99.34 |

### 3.4 SEKTA YA AFYA

Hadi kufikia Machi 2020, Wilaya imekuwa na ongezeko la vituo vitatu vya serikali na vituo 13 vya watu binafsi ikilinganishwa na mwaka 2015 na kufanya Jumla ya vituo vya serikali 18, Taasisi 04, Mashirika ya Kidini 3 na watu binafsi 43. Pamoja na huduma nyingine vituo hivi hutoa huduma za wagonjwa wa nje (OPD), uzazi na watoto, ushauri nasaha na kupima (CTC) na kutoa huduma za afya mashuleni. Mchanganuo wa vituo ni kama ifuatavyo**:-**

**Mchanganuo wa vituo vya Afya kwa mwaka 2020**

| Aina ya kituo | Serikali | Taasisi | Kidini | Binafsi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 1 | 1 | 0 | 1 | **3** |
| Kituo cha Afya | 3 | 1 | 2 | 4 | **10** |
| Zahanati | 14 | 2 | 1 | 17 | **35** |
| Kliniki | 0 | 0 | 0 | 6 | **6** |
| **Jumla** | **18** | **4** | **3** | **43** | **54** |

**Mchanganuo wa vituo vya Afya kwa mwaka 2015**

| Aina ya kituo | Serikali | Taasisi | Kidini | Binafsi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 0 | 1 | 0 | 0 | **1** |
| Kituo cha Afya | 3 | 1 | 2 | 6 | **12** |
| Zahanati | 12 | 3 | 1 | 22 | **28** |
| Kliniki | 0 | 0 | 0 | 2 | **2** |
| **Jumla** | **15** | **5** | **3** | **30** | **43** |

### 3.4.1 Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya

Kwa mwaka 2018/2019, Wilaya iliidhinishiwa na kupokea kiasi cha **Tsh. 1,500,000,000.00.** Fedha yote iliyopokelewa imetumika kujenga majengo 7 tu yaliyokamilika kati ya majengo 22 yanayotakiwa kujengwa kwenye hospitali ya Wilaya. Majengo hayo ni Jengo la utawala, Jengo la wagonjwa wa nje (OPD), Stoo ya dawa, Maabara, Jengo la vipimo vya Mionzi, Jengo la kufulia nguo (Laundry) na Jengo la Wazazi. Mara tu baada ya kupokea fedha, changamoto ya ufinyu wa eneo la mradi lililokusudiwa awali, uwepo wa miamba mikubwa ambayo gharama yake ya kupasua ilikadiriwa kuwa **Tshs. 400,000,000.00** na ingechukua muda mrefu (takribani miezi 4) kukamilisha upasuaji wake. Changamoto hizo zilipelekea mradi kuhamishiwa mtaa wa Isanzu kata ya Bugogwa ambapo Halmashauri ilichukua jukumu la kufidia eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 30.2 kwa gharama ya **Tsh. 176,000,000.00** ukilinganisha na eneo la awali la ukubwa wa ekari 13 tu. Mpaka sasa ujenzi kwa kiwango kikubwa umekamilika majengo yote saba yapo katika




### 3.4.2. Kituo cha Afya Karume

Kituo cha Afya Karume ni kituo cha Afya cha serikali kati ya vituo vitatu vya serikali ndani ya Manispaa ya Ilemela. Kituo hicho kimekuwa na mafanikio makubwa kwenye miundombinu, mapato na huduma hadi kufikia Machi 2020 ikilinganishwa na mwaka 2015. Mwaka 2015 Kituo cha Afya karume kilikuwa na majengo ya wagonjwa wa nje, wanaolazwa, maabara, famasi, jengo la kujifungulia ambalo lilikuwa halitoshelezi kulingana na wateja wanaohudumiwa. Hadi kufikia Machi, 2020 kituo cha Afya Karume kimejenga miundombinu mipya kama, ifuatayo:-

*Jengo la nyumba ya watumishi, Jengo la maabara lenye vigezo stahiki, Jengo la wodi ya wakina mama, Jengo la Kutunzia Maiti(Mortuary), Jengo la Upasuaji na Jengo la huduma za X-Ray na Ultrasound*



Kituo cha Afya cha Karume kinavyoonekana baada ya kukamilika





Nyumba mbili za watumishi katika Kituo cha afya Karume, na choo cha wagonjwa ujezi wake umekailika na zinatumika.

Kwa upande wa mapato, Kituo cha Afya Karume kimefungiwa mfumo wa GoTHOMIS kwaajili ya kutibu wagonjwa kwa njia ya elektroniki ambapo mfumo huo pia unatumika kukusanya mapato ya kituo. Mapato yamepanda kutoka laki tatu (300,000) mpaka milioni moja na laki nne (1,400,000) kwa mwezi.Kwa upande wa huduma katika kituo hiki, Mwaka 2015 huduma zilikuwa zinatolewa lakini si kwa kiwango kikubwa kama sasa. Kutoka 2015 mpaka sasa 2020 huduma zinaonekana kuboreshwa kwani watumishi wameongezeka pia idadi ya wagonjwa wanaopata matibabu katika kituo hiki kwa mwezi imeongezeka kutoka 3000 mpaka 6000.

### 3.4.3 Kituo cha Afya Buzuruga


Kituo cha Afya Buzuruga ni kituo cha Afya cha serikali kati ya vituo vya Afya vitatu ndani ya Manispaa ya Ilemela. Kituo hicho kimekuwa na mafanikio makubwa kwenye miundombinu, mapato na huduma hadi kufikia Machi 2020 ikilinganishwa na Mwaka 2015. Kwaupande wa miundo mbinu, Mwaka 2015 Kituo cha Afya Buzuruga kilikuwa na majengo ya wagonjwa wa nje, wanaolazwa, maabara, famasi, jengo la kujifungulia ambalo lilikuwa halitoshelezi kulingana na wateja wanaohudumiwa.

Mwaka 2015 mpaka 2020 kituo cha Afya Buzuruga kimeboreshwa kwa kujenga miundo mbinu ifwatayo:- *Jengo la nyumba ya watumishi, Jengo la maabara lenye vigezo stahiki, Jengo la wodi ya wakina mama, Jengo la Kutunzia Mait (Mortuary) na Jengo la Upasuaji.*



**Kituo cha Afya cha Buzuruga kama kinavyoonekana kwa juu, baada ya kukamilika ujenzi wake.**

Upande wa mapato, Kituo cha Afya Buzuruga kimefungiwa mfumo wa GoTHOMIS kwaajili ya kutibu wagonjwa kwa njia ya elektroniki ambapo mfumo huo pia unatumika kukusanya mapato ya kituo. Mapato yamepanda kutoka **Tshs. laki tatu (2,000,000)** mpaka **Tshs. Milioni tisa (9,000,000)** kwa mwezi. Kwa upande wa Huduma, Mwaka 2015 huduma zilikuwa zinatolewa lakini si kwa kiwango kama ambacho wateja wanapata sasa. Kutoka 2015 mpaka sasa 2020 huduma zinaonekana kuboreshwa kwani watumishi wameongezeka ambapo kuboreshwa kwa huduma hizo kumesababisha idadi ya wagonjwa wanaopata matibabu imeongezeka kutoka **wagonjwa 4,000 mpaka 12,000** kwa mwezi.



Jengo la OPD katika Kata ya Buswelu ambalo awali ilitegemewa kuwa Hospitali ya Wilaya, kutokana na ufinyu wa eneo Jengo hilo sasa litatumika kama Kituo cha Afya Buswelu.



Uwekaji jiwe la msingi katika Zahanati ya Mtaa wa Lumala Kata ya Ilemela, Ujenzi umefikia hatua ya lenta, lakini huenda ikabadilishwa na kuwa kituo cha afya. Mpaka sasa wametengewa ***Tshs. Milioni 200.***

### 3.4.4 Upatikanaji wa Dawa muhimu

Kufuatia Wilaya kuwa na vituo 18 vya kutolea huduma za afya, upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya umeongezeka kutoka **80% mwaka 2015 hadi 98.3% mwaka 2019.**

### 3.4.5 Uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na Saratani ya matiti

Huduma hii imeendelea kutolewa kwa ufanisi kupitia kituo cha Afya Buzuruga na kwa njia ya mkoba (outreach/mobile services). Hadi sasa, jumla ya akina mama **17,808** wenye umri kati ya miaka 30 mpaka 50 wameweza kupatiwa huduma hii. Jumla ya akina mama **2,432** walikutwa na dalili za awali za saratani ya shingo ya kizazi na kupatiwa matibabu ya tiba mgando (Cryotherapy).Kwa mwaka 2015 akinamama 922 wenye umri kati ya miaka 30 na 50 walifanyiwa uchunguzi wa daily za awali za saratani ya shingo ya kizazi na kati yao 70 walikutwa na dalili za awali za saratani na kupatiwa matibabu (cryotherapy).

Huduma ya uchunguzi wa saratani ya matiti umekuwa ukitolewa katika vituo 26 vinavyotoa huduma ya Afya ya uzazi na mtoto. Huduma hii hutolewa sambamba na huduma za uzazi wa mpango.

### 3.4.6 Mapambano dhidi ya Malaria

Hali ya maambukizi ya Malaria katika Wilaya ya Ilemela kwa sasa ni 6.5%. Kufuatia jitihada kubwa iliyofanywa na Serikali ya awamu ya tano, Maambukizi ya Malaria katika Halmashauri yetu yameweza kupunguwa kwa asilimia 26.5% ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo maambukizi yalikua asilimia 33%. Wilaya imeitikia maagizo ya Serikali katika kupiga vita Malaria kwa kutoa huduma ya matibabu ya ugonjwa wa Malaria katika zahanati 38, vituo vya afya 12 na hospitali 2. Aidha, jitihada zingine zifuatazo zimefanyika katika mapambano dhidi ya Malaria; Ugawaji wa vyandarua vyenye viuatilifu 265,506 ulifanyika kwa jamii

(2015), vyandarua 152,224 Shuleni (2016-Machi 2020), vyandarua 60,198 kwa wajawazito (2016-Machi 2020) na vyandarua 41,512 kwa watoto (2016-Machi 2020), Uhamasishaji wa jamii juu ya usafi wa mazingira, Uhamasishaji wa jamii ili kutambua dalili za Malaria mapema. Aidha, Wilaya imesambaza vipimo vya haraka vya kutambua vimelea vya Malaria (MRDTs) hadi ngazi zote za huduma za afya. Programu hii imesaidia wananchi wengi kupima mara wanapohisi dalili za Malaria kabla ya kumeza dawa kwani "siyo kila homa ni Malaria" na Usimamizi elekezi wa watoa huduma na unyunyiziaji wa viutilifu vya Biolarvicides unaendelea ambapo wilaya imefanikiwa kupokea lita 1181 za viuatilifu. Kabla ya mwaka 2015 tulikuwa na jumla ya zahanati 30, vituo vya afya 9 na hospitali 1 zilizokuwa zinatoa huduma za matibabu ya malaria, aidha hapakuwa na programu za ugawaji wa vyandarua mashuleni na vituo vya afya.

### 3.4.7 Huduma kwa Wazee na watu wenye Ulemavu

Ili kulinda na kuimarisha huduma, wazee **7,312** kati ya lengo la wazee **10,522** wametambuliwa na wanapata matibabu bila malipo. Aidha, ili kuboresha afya ya ngozi kwa watu wenye ulemavu, wastani wa watu wenye ulemavu wa ngozi **115** wamekuwa wakihudumiwa kwa kupewa mafuta ya ngozi kila mwaka.

### 3.4.8 Mapambano dhidi ya UKIMWI

Hali ya maambukizi ya Ukimwi katika Wilaya ya Ilemela kwa sasa ni **7.2%** ikiwa imepungua kwa asilimia **3.8%** ikifananishwa na mwaka 2015 kwani maambukizi yalikua asilimia **11%.** Halmashauri imeendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI.

**Hali ya Maambukizi ya Ukimwi kwa mwaka 2015**

Huduma za upimaji wa VVU kwa wananchi ilikuwa **11,714** kati ya hao waliokutwa na maambukizi ni **1,355** sawa na asilimia **11%,** jumla ya wanaume **4,245** wamefanyiwa huduma ya tohara na waliopimwa maaambukizi ya VVU ni wanaume **2,806** na waliokutwa na maambukizi ni watano (5) Huduma ya kuzuia maambukizi toka kwa mama mjamzito kwenda kwa motto (PMTCT) , wajawazito wapya hudhurio la kwanza **16,633,** waliopima VVU hudhurio la kwanza ni **10,363** na waliokutwa na VVU ni **351**sawa na asilimia **3.4%** Jumla ya wagonjwa 3221 waliweza kuchunguzwa magonjwa ya zinaa wanaume **1,115** na wanawake **2,526**



Ujenzi wa kituo cha magonjwa wa mlipuko kimekamilika na kimeanza kutumika.

### 3.5 Sekta ya Ardhi na Mipango Miji

#### 3.5.1 Urasimishaji Makazi

Ili kudhibiti makazi yasiyo rasmi, Halmashauri inaendelea kutekeleza azma ya Serikali ya awamu ya Tano ya kuboresha makazi yaliyojengwa holela kwa kufanya upimaji shirikishi, ambapo katika zoezi la kurasimisha makazi katika mwaka wa fedha 2019/20, hadi kufikia March 2020 jumla ya Hati miliki za viwanja **10,772** zimeandaliwa na kukamilika kati ya lengo la hati miliki **6,000** ambapo hatimiliki **4,589** ni za maeneo ya urasimishaji Makazi. Jumla ya viwanja **68,000** vya maeneo ya urasimishaji makazi vimebuniwa katika michoro ya Mipangomiji na viwanja **83,352** tayari vimeshapimwa na kupata usajili kwa Mkurugenzi wa Upimaji na ramani. Katika mwaka wa fedha **2015/2016**, Lengo lilikuwa tupime viwanja **16,141** lakini tukafanikiwa kupima viwanja **3,117** tu sawa na **asilimia 19** ya lengo hivyo hadi kufikia **Machi 2020** kumekuwa na mafanikio makubwa katika upimaji wa viwanja na utoaji wa hatimiliki ikilinganishwa na mwaka **2015/16**. Hadi sasa Kata zote **19** zinatekeleza Mpango huu wa kuboresha makazi kwa njia ya Urasimishaji ikihusisha Makampuni **7** ya upimaji yaliyosajiliwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

#### 3.5.2 Miradi ya Upimaji wa Viwanja

1. Ukamilishaji wa upimaji wa viwanja **6,002** katika kata ya shibula katika mradi wa (Muhonze exclusive neighbourhood), kazi ambayo ipo katika **90%** na upimaji umekamilika ambapo michoro ya upimaji imewasilishwa Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuidhinishwa na kisha kutangazwa kwa ajili ya kuuza viwanja.

2. Mradi wa upimaji wa Viwanja **1,700** katika kata ya Sangabuye eneo la Nyafula, Upimaji umekamilika kwa **85%** ambapo jumla ya viwanja **760** vimeshapimwa na ramani zimeshaidhinishwa na wizara ya ardhi na uthamini umeshafanyika. Aidha, ramani ya viwanja **940** imeidhinishwa. Kwa sasa Manispaa ipo katika hatua ya Ulipaji wa Fidia.

3. Kazi ya Upimaji katika kata ya kiseke ipo katika hatua ya uidhinishaji katika wizara ya Ardhi nyumba na maendeleo ya Makazi ambapo Jumla ya viwanja **4,267** vimeidhinishwa hivi karibuni kwa kuwa kazi ya uwandani (site work) imekamilika.

4. Mradi wa upimaji viwanja 1200 katika eneo la Nyamadoke umekamilika na tayari Halmashauri ilitangaza kuuza viwanja hivyo na hadi Machi 2019 mapato ya mauzo ya viwanja yalikuwa bilioni 1.7 ambazo zilitumika katika kulrejesha fedha zilizotolewa na Wizara ya Ardhi kiasi cha **Tsh. 1,550,000,000.00** fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utaratibu wa kuzitumia katika miradi ya upimaji wa viwanja na kulipa fidia (Revolving Fund) kisha kuzirejesha baada ya kuuza viwanja.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Ndugu Richard Kwitega akipokea Hati yake toka kwa Naibu Waziri Dkt. Angeline Mabula, kwa mbali ni Ndugu Kamiyanda Afisa Mipango Miji Mkoa wa Mwanza.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha Ndugu Richard Kwitega akipokea Hati yake toka kwa Naibu Waziri Dkt. Angeline Mabula, kwa mbali ni Ndugu Kamiyanda Afisa Mipango Miji Mkoa wa Mwanza.



Pamoja nakugawia wananchi wengine Hati za umiliki wa ardhi Mbunge wa Jimbo Dkt. Angeline S.L. Mabula, nae alipata fursa yakukabidhiwa Hati yake ya umiliki wa ardhi na Msajiri wa Hati Mkoa wa Mwanza Ndugu Ivan.

### 3.5.3 Migogoro ya Ardhi

Ofisi ya Mbunge, Mkuu wa Wilaya, Mstahiki Meya, Mkurugenzi tumekuwa na utaratibu wa kupokea kero zinazohusiana na migogoro ya ardhi kwa kushirikiana na wataalam wa Mipango miji jambo linalopelekea migogoro mingi ya ardhi kupatiwa ufumbuzi kwa haraka.

Aidha namshukuru sana Mkurugenzi wa Manispaa na watendaji wote wa idara ya ardhi wakiongozwa na ndugu Shukurani Kyando, kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya na hatimae kuifanya Mansipaa ya Ilemela kutokuwa na changamoto mpya za migogoro ya ardhi. Halmashauri imekuwaikipokea na kushughulikia migogoro mbalimbali ya ardhi ihusishayo Taasisi na wananchi, wananchi na wananchi na migogoro ambayo imekuwepo kabla ya kuanzishwa kwa Halmashauri mwaka. 2012.

Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Ilemela imeshirikiana kwa karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mh. Mbunge na ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi katika kuhakikisha migogoro ya ardhi inamalizika. Mnamo tarehe 13/9.2017 Mhe. Mkuu wa Mkoa alifika katika viwanja vya Halmashauri ya Ilemela ambapo migogoro 139 ya ardhi ilipokelewa na yote imefanyiwa kazi na kumalizika.

Halmashauri kupitia Idara ya Mipango Miji kwa kushirikiana na Mhe. Mbunge hufanya ziara na ukaguzi wa maeneo katika kata mbalimbali ambapo ndani ya miaka mitatu migogoro **195** ilipokelewa na kushughulikiwa, lakini pia Idara ya Mipango miji imetenga siku za **Jumatatu na Alhamisi** kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi ofisini na siku za **Jumanne, Jumatano na Ijumaa** kutembelea Kata ili kuyafikia maeneo yenye Migogoro/malalamiko kwa ajili ya kuitatua kwa kushirikiana na viongozi wa Kata na Mitaa husika. Mpaka kufikia Februari, 2020 Halmashauri imefanikiwa kumaliza migogoro yote ya baina ya mtu na mtu na baina ya Taasisi na Serikali kwa **asilimia 95** na kubakia na migogoro michache inayohusu fidia.

i. Migogoro yakurithi toka Halmashauri ya Jiji la Mwanza ya utwaaji wa maeneo kwa ajili ya uanzishwaji wa shule na kata kwa ahadi ya kulipa fidia lakini mpaka mwaka 2012 Jiji lilipokuwa linagawanywa fidia hizo zilihamishwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

ii. Migogoro katika maeneo ya miradi ya viwanja vya Buswelu, Nyamhongolo, Kiseke na Kabuhoro ambapo viwanja vilipimwa na kuuzwa bila wamiliki wa awali kulipwa fidia zao. Madeni yote ya fidia yalihamishiwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela wakati viwanja tayari vilikwisha uzwa na kumalizika. Madeni yote yanafikia kiasi cha **shilingi 4,600,000,000.00.**

**MIGOGORO MIKUBWA ILIYOSHUGHULIKIWA NA SERIKALI.**

I. Mgogoro wa eneo la Jeshi na wananchi eneo la Ilemela Nyagunguru, Serikali ilifanya uthamini na uhakiki wa mali za wananchi **369** na kulipa fidia jumla ya **shilingi 3,534,295,165.58.**

II. Mgogoro baina ya wananchi na Jeshi la wananchi wa Tanzania (JWTZ) eneo la Kata ya Kahama katika mitaa ya Lukobe, Kahama, Nyanguku na Buduku. Uthamini umefanyika na zoezi la uhakiki linaendelea kufanyika ambapo jumla ya **shilingi 6,195,113,000.00** zinatarajiwa kulipwa ili kutanua maeneo ya Jeshi kwa lengo la kuimarisha ulinzi wa maeneo ya uwanja wa ndege.

III. Eneo la Kigoto, mgogoro wa wananchi na jeshi la polisi ambapo mgogoro huo umepatiwa ufumbuzi wa wananchi kurasimishiwa maeneo yao pamoja na mengine kupatiwa Jeshi la polisi.

IV. Mgogoro wa Mhonze uliodumu kwa miaka zaidi ya 13 lakini ulimalizika kupitia upimaji shirikishi, wananchi wamepimiwa maeneo yao. Jumla ya viwanja **8,300** vimepimwa kwa makubaliano ya asilimia 85 anachukua mwananchi na 15% Halmashauri, zoezi limefanyika vizuri.

V. Mgogoro kati ya Wananchi wa Jiwe kuu na kampuni ya Maswe drill umemalizika japokuwa kuna tetesi maswi Drill amekimbilia mahakani.

VI. Wananchi wa Nsumba na Mradi wa Mkoa, eneo lilipima viwanja na kugawiwa watumishi wa Serikali bila ridhaa ya wananchi, wamerudishiwa maeneo yao.

VII. Wananchi wa Nyasaka na Viwanja vyao.

VIII. Viwanja vya wananchi Bwiru Elimu watamilikishwa viwanja vyao baada ya tapeli Lazaro na kundi lake kushindwa kesi.



**Moja ya ziara katika maeneo yaliyokuwa yamevamiwa na wanachi ambayo wizara imeridhia wananchi warasmishiwe. Katika picha ni moja ya ziara kata ya Ilemela eneo la mwambani.**

### 3.5.4 Ukusanyaji wa kodi ya Ardhi

Halmashauri imeendelea kufanya vizuri katika ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi kwani kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi kufikia Machi 2020 Halmashauri imefanikiwa kukusanya **Tsh 2,045,895,021.74** kati ya Lengo la **Tsh 3,000,000,000** Ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2015/16 ambapo Halmashauri ilikusanya **Tsh. 1,925,000,000.69** kati ya lengo la **Tsh 1,500,000,000.00**. Mwenendo wa ukusanyaji wa kodi hiyo kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2020 umeonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:-

**Ukusanyaji wa Kodi ya Aridhi tokea Mwaka 2015 hadi March 2020**

| MWAKA WA FEDHA | LENGO | KIASI KILICHOKUSANYWA | % |
|---|---|---|---|
| 2015/16 | 1,500,000,000.00 | 1,925,000,000.69 | 128 |
| 2016/17 | 2,500,000,000.00 | 2,618,883,965.47 | 105 |
| 2017/18 | 2,500,000,000.00 | 2,812,969,266.11 | 113 |
| 2018/19 | 3,000,000,000.00 | 2,903,513,648.38 | 97 |
| 2019/20 - Machi | 3,000,000,000.00 | 2,045,895,021.74 | 68 |

### 3.6 Sekta ya Maji

Jimbo la Ilemela ni wanufaika wakubwa wa mradi wa Serikali ya kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) ambao unatekelezwa katika Miji na Wilaya zifuatazo kupitia Programu ya uboreshaji wa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza, Miji ya Bukoba na Musoma, Miji Midogo ya Misungwi, Magu na Lamadi. Programu hii inajulikana kama "Lake Victoria Water and Sanitation (LVWATSAN)" ambao unatekelezwa chini ya Ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao ni Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank, EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Francaise de Development, AFD) kwa gharama ya **TZS. Billion 276.925 (Euro Milioni 104.5)**. Katika Manisipaa ya Ilemela watekelezaji ni Mkandarasi Kampuni ya M/s. JOS. HANSEN & SOEHNE GmbH in JV with M/s. JR INTERNATIONAL BAU GmbH kutoka Ujerumani kupitia Mkataba Na AE/042/2015-2016/W/01 kwa gharama ya **Euro. 14,689,448.35 (**sawa na **TZS Billioni 38.927)**. Mkataba wa utekelezaji wa shughuli za miradi ulisainiwa tarehe 16 Februari 2017 baina ya MWAUWASA na Mkandarasi. Utekelezaji wa kazi za Ujenzi wa Mradi zilianza rasmi tarehe 26 Mei 2017. Katika Manispaa ya Ilemela. Kazi za mradi wa maji zinategemea kumalizika mwishoni mwa mwezi Mei. Kwa ujumla miradi hii imeshaanza kutumika/kutoa huduma kwa wananchi husika.

Kazi zinazofanyika kupitia miradi hii ni kama zilizobainishwa hapa chini:

**A: MRADI WA MAJI**

**NYASAKA** Kazi zilizofanyika na kukamilika ni ulazaji wa mabomba kilomita **19.4** yenye ukubwa wa DN (200, 160, 110, 90, 63, 50) Gharama ya **Tshs. 1,615,500,00/=.** Ulazaji wa bomba kuu la kupeleka maji kwenye tanki kutokea kituo cha kusukuma maji Kitangiri kilometa 1.8 lenye ukumba na DN 200, **Tshs. 291,500,000,** Ulazaji wa nomba kuu kupeleka kituo cha kusukuma maji tokea Nyashana kilometa 2.2 lenye ukubwa wa DN450, kwa gharama ya **Tshs 2,252,500,000/=** Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa mita za ujazo **1,200 (lita 1,200,000)** kwa gharama ya **Tshs. 715,500,000/=** na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji Nyasaka chenye uwezo wa kusukuma maji mita za ujazo 128 kwa saa na kisima mita za ujazo **55 (lita 55,000)**



*Tanki la kuhifadhia Maji lenye ujazo wa mita 1200 sawa na lita 1,200,000 za maji lililojengwa eneo la Nyasaka tayari limekamilika na maji yameanzwa kusambazwa maeneo mbalimbali ya Jimbo.*

**MJIMWEMA:** Kazi zilizofanyika na kukamilika ni ulazaji wa mabomba kusambazia watu kutoka katika kutupeleka katika kituo kikuu cha kusukuma maji na ujenzi wa taki kuhifadhia maji lenye ujazo wa mita 1200 (Sawa lita 1,200,00) kazi zote imeamilika.

**KITANGIRI /IBANDA:** Kazi zilizofanyika na kukamilika ni ulazaji wa mabomba kilomita 11.6 yenye ukubwa wa DN (200, 160, 110, 90, 63, 50) Gharama ya Tshs. 715,500,000/=. Ulazaji wa bomba kuu la kupeleka maji kwenye tanki kutokea kituo cha kusukuma maji Kitangiri kilometa 1.8 lenye ukumba na DN 150, Gharama ya Euro 291,500,000 na Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa mita za ujazo 500 (lita 5,000) gharama Euro 165,000 na ujenzi wa kituo cha kusukuma maji chenye uwezo wa kusukuma mita za ujazo 64 kwa saa na kisima chenye ujazo wa mita 55 (lita 55,000) kwa gharama ya Euro 160,00

Mradi umekamilika kwa asilimia 98 % ,Na sasa upo kwenye majaribio



**Tanki la kuhifadhiaMaji lililojengwa Ibanda Kata ya Kirumba lenye mita za ujazo 500 sawa na lita 5,000**

**NYAMHONGOLO:** Ujenzi wa Tenki la kuifadhi maji wenye ujazo wa mita za ujazo 500 (lita 500,000) kwa gharama ya **Euro 150,000** na kazi imekamilika

**KIRUMBA-MWALONI**: Shughuli zilizofanyika ni kuondoa Mabomba chakavu/Zamani na kuweka mapya) Kazi zilizofanyika na kukamilika ni Ulazaji wa mambomba ya kusambaza maji kilomita **11.7** yenye ukumbwa DN(200,160,110,90,63,50) gharama ya **Euro 728,000.**

**B: MRADI WA KUONGEZA MTANDAO WA MAJITAKA**


**Kilimahewa/Isamilo:** Kazi zilizokamilika ni Ulazaji wa mambomba ya kukusanya majitaka kilomita **0.8** yenye ukumbwa DN(250) na Bomba za kukusanya maji kwa wateja kilomita **0.79** kwa wateja wapy **37** kwa gharama ya **Euro 265,000**

**C: UJENZI WA VYOO MASHULENI NA MAENEO YA KUTOLEA HUDUMA KWA UMA.**

Tulipokea mradi huu kwa awamu ya pili baada ya awamu ya kwanza kukamilika katika shule za msingi na maeneo ya huduma. Tunaishukuru sana Serikali kwa msaada huu uliotolewa kupitia MWAUWASA:



Moja ya tanki la maji katika mradi wa maji wa Viji 10 ambao ulisimama tangu 2012, awamu ya 5 umekamilika kama unavyoonekana. Tanki lina lita za ujazo 5,000




Moja ya vyoo vya kisasa kabisa vilivyojengwa na MWAUWASA awamu ya kwanza katika shule za msingi 10 Jimboni Ilemela

hapo chini. Mkandarasi aneyefanya kazi ya ujenzi wa vyoo mashuleni na maeneo ya kutolea huduma kwa uma ni URISO Kutoka dar es salaam na jumla ya Tsh 2,306,386.98 pamoja na VAT, zitatumika katika hutekelezaji wa mradi huu, Mradi ulianza tarehe 16 Marchi 2020 na Kukamilika Marchi 2021.

**Mchanganuo wa ujenzi wa vyoo awamu ya pili ni kama ufuatavyo na kazi zinaendelea;**

**Nyamhongolo Shule ya Msingi** – Choo kikubwa (Generic Model toilet) Matundu 20, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM). **Kilimamani shule ya Msingi** – Choo cha kati (Basic Model toilet) - Matundu 12, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na Kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM. **Muungano shule ya Msingi** – Choo kikubwa (Generic Model toilet) Matundu 20, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM). **Kaselya shule ya Msingi** - Choo kikubwa (Generic Model toilet) Matundu 20, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM). **Nyasaka shule ya Msingi** - Choo cha kati (Basic Model toilet) - Matundu 12, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na Kichoma taka ngumu na hatalishi( ( Incinerator for MHM. **Nyamwelekelwa Shule ya Msingi** - Choo kikubwa (Generic Model toilet) Matundu 20, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM). **Nsumba shule ya Msingi** - Choo kikubwa (Generic Model toilet) Matundu 20, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM). **Mwenge shule ya Msingi** - Choo cha kati ( Basic Model toilet) - matundu 12. **Mjimwema Shule ya Msingi** - Choo cha kati (Basic Model Toilet) - Matundu 12 na Kichoma taka ngumu na hatalishi( ( Incinerator for MHM). **Kiloleni Shule ya Msingi** - Choo cha kati (Basic Model Toilet) - Matundu 12, Choo cha walimu na walemavu matundu 3 na Kichoma taka ngumu na hatalishi (Incinerator for MHM). **Pasiansi Shule ya Msingi** - Choo cha walimu na walemavu matundu 3. **Buzuruga Dispensary** - Choo cha kati (Public Model Toilet) - Matundu 12. **Nyakato Dispensary** - Choo cha kati (Public Model Toilet) - Matundu 12.




Moja ya vyoo vya kisasa kabisa vyilivyojengwa na LVEMP katika Shule za Msingi tatu Buzuruga, Nyambiti na Isenga Jimboni Ilemela.



Sehemu ya majengo yaliyojengwa katika chanzo cha Maji eneo la Kabangaja Kata ya Bugongwa, ujenzi na ufungaji pumpu yakusukuma maji umekamilika.



Enjinia Anna akijaribu kusogeza mpira wa maji eneo la Kabangaja mahali ilipojengwa Cjanzo cha maji kuelekea tanki la Igogwe na Kabangaja yenyewe.



Moja wa mafundi bomba akiendelea kupima maeneo ambayo usambazaji wa mipira ya maji.



Moja ya hatua iliyochukuliwa na MWAUWASA kujenga matanki ya Maji eneo la NYABUSALU na NSUMBA kwa muda kwa ajili ya wananchi kupata maji wakati Mradi mkubwa unaendelea kujengwa. Katika Picha Diwani wa Kata ya Kiseke Mhe. Innocent akimtwisha maji mmoja wa wananchi wake.



Kisima kirefu cha maji kilichojengwa kwa ufadhili wa UBALOZI WA CHINA eneo la IGOGWE Kata ua Bugogwa Mradi umekamilika Kisima kinahudumia Mitaa minne (Igogwe, Isanzu, Kirino na




Kisima kirefu cha maji kilichojengwa kwa msaada wa kampuni ya bia ya Serengeti kwa ushirikiano na taasisi ya ANGELINE FOUNDATION. Kisima kinahudumia mitaa minne (Kaguhwa, Iwelyashinga, Iramba B na Ikigijo) katika kata ya Nyamhongolo




Moja kati ya Visima vifupi 7 vilichojengwa na Taasisi ya MUSLIMS AGENCY TANZANIA OFFICE Mtaa wa CHABAKIMA Kata ya SHIBULA

**UANZISHWAJI WA MAMLAKA YA MAJI VIJIJINI (RUWASA)**

Napenda kuishukuru sana Serikali ya awamu ya tano kwa kugusa maisha ya mtanzania wa chini kabisa. Maji ni uhai, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ndani ya jimbo. Awali kabla yakuanzishwa ka RUWASA Jimbo lilikuwa likipata huduma kupitia MWAUWASA na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemelakupitia idara yake ya maji. Idara hiyo kwa sasa haipo tena, kuna miradi mitano iliyokuwa chini ya Miradi ya Vijiji 10 ambapo Manispaa ilipata visima 8 kati ya hivyo ni visima viwili tu vimekamilika vingine bado. Gharama yote ya mradi wa visima 10 ilikuwa **Tshs. 6,040,564,084** pesa zilizolipwa hadi sasa ni **Tshs 4,606,989,816.00** tu. Hivyo jumla ya **Tshs 1,433,574,268.21** zinahitajika ili kukamilisha utekelezaji wa miradi hii. Miradi hii ikikamilika itanufaisha jumla ya wakazi **59,073** katika mitaa **39**. Aidha, ili kuwezesha uendelevu wa miradi ya maji, Halmashauri imeunda Jumuia ya Watumia Maji moja na nyingine **9** zinaendelea kuundwa na zitapatiwa mafunzo ili kuziwezesha kusimamia na kuendesha miradi ya maji.

## 3.7 Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi

### *3.7.1* Mikopo ya wanawake na vijana

Kuanzia Mwaka 2015 hadi Machi 2020, Halmashauri imeendelea kuviwezesha vikundi vya Wanawake na Vijana ambapo jumla ya **Tshs. 1,431,000,000.00** zimekopeshwa kwa vikundi 539. Kumekua na Mwamko mkubwa kwani mwaka 2015 Halmashauri ilikopesha vikundi 17 tu kiasi cha **Tsh 22,000,000** lakini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi Machi, 2020 jumla ya vikundi 166 vimekopeshwa jumla ya **Tsh 540,000,000.00.** pesa iliyoko katika mzunguko ni **Tshs. 600,000,000**

| MWAKA | KIASI TOLEWA | WANAWAKE | | VIJANA | | WALEMAVU | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KIASI | VIKUNDI | KIASI | VIKUNDI | KIASI | VIKUNDI |
| **2015/2016** | 22,000,000 | 13,000,000 | 11 | 9,000,000 | 6 | 00 | 00 |
| **2016/2017** | 252,000,000 | 181,000,000 | 90 | 71,000,000 | 35 | 00 | 00 |
| **2017/2018** | 116,000,000 | 103,000,000 | 42 | 13,000,000 | 6 | 00 | 00 |
| **2018/2019** | 501,000,000 | 397,000,000 | 145 | 92,000,000 | 33 | 12,000,000 | 5 |
| **2019/2020** | 540,000,000 | 418,000,000 | 126 | 101,000,000 | 32 | 21,000,000 | 8 |
| **JUMLA** | **1,431,000,000** | **1,112,000,000** | **414** | **286,000,000** | **112** | **33,000,000** | **13** |

**NB:** Bajeti ya mwaka **2020/2021** Manispaa imetenga **Tsh. 857,349,400,00** mgawanyo wake utakuwa kama ifuatavyo **4%** wanawake **Tshs.342,939,760.00, 4%** ya Vijana **Tshs.342,939,760.00** na **2% Tshs.171,469,880.00**

Mafanikio katika suala la utoaji mikopo kwa makundi maalumu imekuwa ikitolewa baada ya kutoa semina kwa wakopaji ili kuepusha matumizi ya mikopo nje ya makusudio.



Afisa Maendeleo Manispaa ya Ilemela Ndugu Sitta Singibadi akitoa mada juu mikopo ya mikopo ya 10% inayotolewa na Manispaa kwa viongozi wa wanawake.



Ziara ya Mbunge kuongea na Vikundi vya Wajasiliamari kata ya Kamekame akina mama



Moja ya vikundi ya vijana wa bodaboda toka Kata ya Nyamhongolo walionufaika na mikopo ya vijana, nihovyo kuweza kumiliki pikpiki zao wenyewe.



Mmoja wa wawezeshaji toka taasisi ya Kivulini Ndugu Yunice Mayengela akitoa mada juu Nafasi ya mwanawake kumiliki ardhi kisheria. Walioko meza kuu kutoka kushoto ni Meneja wa Azania benki Ndugu Sasa, Mkuu wa Idara ya Ardhi Ndugu Kyando, Mbunge wa Jimbo Dkt Angeline na Mwenyeketi wa UWT Wilaya Ndugu Salome Kipondya.

### 3.7.2 Uanzishwaji wa jukwaa la wanawake

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilifanikiwa kuanzisha Jukwaa la wanawake **mwaka 2017,** ambalo hadi kufikia **mwaka 2020** Jukwaa lina jumla ya **wanachama 5,685** ukilinganishwa na **wanachama 153** kipindi lilipoanzishwa. Jukwaa hili linawaleta pamoja wanawake wajasiliamali wa Wilaya ya Ilemela.

### 3.7.3 Uwezeshaji kiuchumi kaya masikini

Mpango wa kunusuru kaya maskini - TASAF ulianza kutekelezwa Mwaka 2014 kwa utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini. Uhawilishaji wa fedha ulianza **Mwezi Julai, 2015** katika **mitaa 69** kukiwa na walengwa **4,807.** Mpaka kufikia **Machi 2020** Jumla ya **Tsh. 4,094,694,600** zimepokelewa kwa ajili ya kuhawilishwa kwa kaya maskini na usimamizi katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Mitaa. Jumla ya **Tsh. 3,880,780,200** zimehawilishwa na **Tsh. 231,914,400** zilirejeshwa TASAF kwa kutochukuliwa na walengwa wakati wa malipo. Kaya zinazonufaika na mpango huu ni kaya **3,838** kufikia **Machi 2019.** Sababu ya kupungua kwa kaya ni kuondolewa kwa kaya amabazo hazikua na sifa ya kua kwenye mpango. Zoezi la uhakiki wa kaya limekuwa likifanyika ili kubaini kaya zisizo na sifa na kuziondoa katika mpango ili kuweza kupata tija kwa kaya zinazostahili na kufikia malengo ya mpango. Kufikia Machi 2020, uhakiki ulifanyika katika mitaa yote 69 na jumla ya **kaya 969** ziliondolewa kwa kutokuwa na sifa ya kuwemo kwenye mpango. Kaya hizi zilikuwa zimepokea kiasi cha **Tsh.110,616,000.00** na ziliandikiwa barua ya kurejesha fedha walizopokea. Kiasi cha **TSh. 516,000.00** kimerejeshwa. Uhuishaji wa taarifa za kaya hizi umefanyika na kubaini kaya zinazopatikana na zinaweza kulipa deni ni **130** zikidaiwa **Tsh. 57,890,000.00** na Ufuatiliaji unaendelea kufanyika.

### 3.8 Mpango wa uboreshaji wa Makazi

Katika kutafuta namna bora ya kuharakisha maendeleo katika Jimbo la Ilemela, nilichukua hatua ya kutafuta marafiki kwa ajili ya kushirikiana nao. Kupitia urafiki wa miji dada Jiji la DEAGU ya Korea ya Kusini na Manispaa ya Ilemela, kumekuwa na ushirikiano wa pamoja wa kuendesha program ya maendeleo ya vijiji vya mfano. Shughuli hii inatekelezwa katika mitaa miwili ya *Ihalalo kata ya Sangabuye na Iponyabugali kata ya Kayenze.* Mpaka sasa viongozi 10 walipatiwa mafunzo juu ya mradi huu na Jamhuri ya Watu wa Korea Kusini wameahidi kuanza kuviendeleza kwa kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na makazi bora. Pia, nchi ya Korea Kusini imeipatia Wilaya yetu kiasi cha **Tshs. 136,100,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Ihalalo ambapo ujenzi ulikamilika na shule tayari imefunguliwa. Aidha, Halmashauri imemaliza kutekeleza Mpango huu kwa kujenga vyumba vya 3 vya madarasa ambapo jumla ya **Tshs. 190,100,000** zilizo tolewa na nchi ya Korea Kusini kwa ajili ya Kazi hiyo zimetumika.

### 3.9 Sekta ya Viwanda

Halmashauri katika kutekeleza sera ya viwanda imebainisha maeneo mawili ya uwekezaji wa viwanda ambapo eneo la Nyamhongolo lenye ukubwa wa **hekta 72.7** linaandaliwa mpango kabambe na eneo la Ihalao lenye ukubwa wa **ekari 650** yametengwa kwa ajili ya kanda Maalumu ya Kiuchumi. Maeneo haya yatamilikiwa na Halmashauri na hivyo kuwa chanzo cha kuiongezea kipato Halmashauri katika siku zijazo. Andiko mradi la takribani Tshs. **492,000,000,000.00** limeandaliwa na upembuzi yakinifu kwa ajili ya eneo la uwekezaji wa Viwanda "Nyamhongolo Industrial Park" limekamilika na linatarajiwa kupelekwa Wizara ya Fedha kupitia OR – TAMISEMI kwa ajili ya kupatiwa fedha za Miradi ya Kimkakati. Hii ni baada ya Manispaa yetu kukubaliwa maombi ya Miradi Mikakati ya Stendi ya Mabasi na Maegesho ya Malori inayotekelezwa kwa gharama ya **bilioni 28.** Vile vile, Halmashauri kwa kushirikiana na sekta binafsi kwa mwaka **2017/2018** pekee, ilifanikiwa kuanzisha viwanda **24**. Kati ya viwanda hivyo vya kati ni **6** na vidogo ni **18**.

### 3.10 Sekta ya Barabara

**Mtandao wa Barabara:** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Manispaa ya Ilemela inahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya **Km 870.22**, barabara za lami **Km 37.84** sawa na asilimia **4.4**, barabara za zege **km 1.78** sawa na asilimia **0.21**, barabara za mawe **km 2.48** sawa na asilimia **0.28,** barabara za changarawe **km 75.21** sawa na asilimia **8.6** na barabara za udongo **km 752.91** sawa na asilimia **86.51.** Barabara hizi zimekuwa zikihudumiwa na fedha za mfuko wa barabara (Road Fund) pamoja na makusanyo ya ndani ya Halmashauri. Barabara nyingi za udongo hupitika kwa shida wakati wa mvua. Halmashauri ya Manispaa kupitia fedha zake za makusanyo ya ndani kila mwaka imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kuzikarabati na kuzifanya zipitike. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri kupitia wakala wa barabara Mjini na Vijijini (TARURA) inaendelea na mkakati wa kujenga mitaro ya barabara ambayo itapunguza gharama za ukarabati wa mara kwa mara kutokana na jiografia ya mazingira ya mji kuwa una vilima na milima.

#### 1. UTEKELEZAJI WA MIRADI 2017/2018

Matengenezo ya Mara kwa mara (Routine Maintenance) (Uzibuaji wa mitaro na Makalavati) Barabara mbalimbali Manispaa ya Ilemela (Bwiru, Furahisha, Mecco, Mkudi, Kitangiri, Vijana, Penda, Kiyungi – Kirumba, NHC – Gedeli, KVCC,Vijana-Msikitini, Lakairo,Mliman-Kirumba, TTCL, Tupendane, Karume - Kifua wazi, Bismark - Kirumba, Ibungilo na Mnyampala - terrazo) jumla ya **TShs 50,521,400.00** zimetumika na kazi imekamilika

Matengenezo ya Maeneo Korofi (Spot Improvement) barabara za Ilemela – Mahakaman Km 1.00 na Buswelu - Bujingwa Km 4.5 gharama **Tshs. 106,743,242.00**

Matengenezo ya Maeneo Korofi (Spot Improvement) barabara za Isesa s/msingi – Ngw'vila Km 1.5, Kahama – Igombe Km 4.5 na Nyafula – Igumamoyo Km 2.0 gharama **Tshs.145,996,921.90**

Kwa kipindi kifupi tangu TARURA ianzishwe, kazi nyingi zimefanyika kama itakavyoonekana hapa chini:

Matengenezo ya muda maalumu (Periodic Maintenance) barabara za Nyamuge – Nyasaka centre (Barabara ya mawe) (0.2km) Manispaa ya Ilemela gharama **Tshs. 76,048,244.70** kazi imekamilika.



**Barabara ya Mawe kutoka Nyamuge hadi Nyasaka Center**

Matengenezo ya maeneo korofi (Spot Imrovement) barabara za Nyambiti **Km 2.5** na PPF –Nyakurunduma **Km 1.3** gharama ya **Tshs. 159,222,800/=** kazi imekamilika.



Mitaro inayoendelea kujengwa katika Barabara ya PPF – Nyakurunduma.




Daraja la Nyamhongoro – Kashishi limekamilika na linatumika, aidha daraja linatuunganisha na Wilaya ya Nyamagana.

Matengenezo ya muda maalumu barabara ya mawe ya Tupendane (0.5km) gharama ni Tshs. 163,000,000/=

Matengenezo ya daraja la Nyamhongolo - Kashishi gharama **Tshs. 124,280,946.78** kazi imekamilika.



Barabaya ya Tupendane Km 0.5 inayojengwa kwa Mawe kazi ujenzi umefikia 70% kazi inaendelea.



Muonekano ya barabara mpya ya Sabasaba – Kiseke – Buswelu Km 9.2 inavyoonekana usiku.

Ujenzi wa Kaivat katika barabara la Mecco – TFDAKm 0.87 na Matengenezo ya Muda Maalum barabara ya National – Gedeli Km 0.68



Matengenezo ya Sehemu Korofi barabara ya Igogwe – Isanzu – Kabusungu –Igumamoyo – Sangabuye Sekondary **Km 8.73** na Matengenezo ya Muda Maalum barabara ya Kahama – Igombe **Km 9.2** na Buswelu – Cocacola **Km 3.2** gharama **Tshs 158, 581, 223.00**



**Kalavati barabara ya Isanzu-Igumamoyo-Kabusungu-Sangabuye ujenzi umefikia asilimia 50 kazi inaendelea. Ujenzi utakamilika 30.6.2020**

Matengenezo ya Madaraja Barabara ya Nundu – Kanisani, NHC – Kigala na Kigala – Lagos – Kiseke CCM gharama ya mradi ni **Tshs. 112,210,000.00**



Ujenzi wa daraja NHC Kigala ujenzi umefikia asilimia 65 ujenzi unatarajiwa kukamilia 30.6.2020.

**MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MATENGENEZO YA BARABARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

- Matengenezo ya mara kwa mara ya Kuzibua na Kusafisha Mitaro kwenye Barabara Mbalimbali Manispaa ya Ilemela (Desilting) gharama ya mradi **Tshs 67,740,000/=**

- Matengenezo ya mara kwa mara ya Kuziba mashimo na kuweka alama za barabarani katika Barabara za Lami za,Mecco,Furahisha na Sanga Kiloleli na Matengenezo ya Muda maalumu Barabara ya Sabasaba gharama yake **Tshs. 59,135,000/=**

- Matengenezo ya Muda Maalum barabara za Kahama – Igombe **(9.12Km),** Kahama - Isela - Masemele - Ihalalo - Isela - Nwangvila **(14.4Km),** Nyamilolelwa - Bukala - Butindo - Ibaya - Ilalila **(5.67Km)** na Matengenezo ya Sehemu Korofi barabara za Igogwe - Kabusungu - Igumamoyo - Sangabuye Sec **(8.73Km),** Igombe - Ziwani **(0.32Km)** Gharama **Tshs 181,480,000/=**

- Matengenezo ya Sehemu Korofi barabara za Ilemela – Mahakamani **(1.3Km),** Kalamba – Msumbiji – Msumbiji – PPF Kiseke **(2.5Km),** Bigbite Michungwani **(1.3Km),** Nyasaka Shops (Jabal hilali – Nyasaka Sokoni) **(1.1Km),** Mkudi **(0.25Km),** Ibungilo **(0.8Km),** Gharama ni **Tshs 225,000,000/=**

- Matengenezo ya Sehemu Korofi Barabara za Mecco – Kangae – Buswelu **(2.81Km),** Nyamilekelwaa – Nundu **(1.4Km),** Gedeli – Kangae **(0.95Km)** na Matengenezo ya muda maalumu barabara za National – Gedeli **(0.68Km),** Buzuruga – Mitimirefu – Makaburini **(1.13Km).** Gharama **Tshs 167,954,000/=**

- Matengenezo ya Sehemu Korofi Barabara za Kiyungi – Kirumba **(0.5Km),** Greenview – PPF Kiseke **(1.31Km),** Airport – Pasiansi (Sunrise) **(0.59Km)** na Matengenezo ya muda maalumu barabara za Jiwe Kuu (Stone Pavement) **1.1Km,** Breweries **(2.5Km)** na Mwanasheria **1.1Km** Gharama **Tshs.187,476,000/=**

- Matengenezo ya Sehemu Korofi Barabara za Buselu - Nyamadoke – Nyamhongolo **(9.6Km),** Nyamhongolo Viwandani - Nyamhongolo Centre **(2.2Km)** na Matengenezo ya muda maalumu barabara za Buswelu - Cocacola **(3.38Km),** Buswelu - Bujingwa - Buyombe - Kiseke **(6.0Km)** na Angeline Mabula Sec. Gharama **Tshs. 170,240,000/=**

- Matengenezo ya Madaraja Barabara ya Bwiru, Lumala, Butindo na Buduku, gharama za mradi **Tshs.121,903,000/=**

## ORODHA YA BARABARA ZINAZOTEGEMEWA KUTENGENEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Zifuatazo ni barabara ambazo zinategemea kuanza kutengenezwa ifikapo Julai 2020: Matengenezo ya kawaida katika barabara mbalimbali zenye urefu wa Km 84.68

Barabara ya Furahisha km 0.65, Kitangiri km 0.64, Penda km 0.92, Bwiru Km 4.10, Mecco km 1.47, Sanga - Kiloleli Km 1.9, Pasiansi - Buzuruga km 7.87 Tunza Loop km 4.77, Igogwe - Kabusungu - Igumamoyo - Sangabuye Sec Km 8.73, Igombe - Ziwani km 0.32, Kahama - Igombe km 9.12, Kahama - Isela - Masemele - Ihalalo - Isela - Nwangvila km 14.4, Nyamilolelwa - Bukala - Butindo - Ibaya - Ilalila km 5.67, Ilemela - Mahakamani km 1.3, na barabara ya Kalamba - Msumbiji - Msumbiji - PPF Kiseke km 2.5,


Matengenezo ya muda mfupi Spot Improvement Works Barabara ya Ilemela - Mahakamani Km 1.3, Kalamba - Msumbiji - Msumbiji - PPF Kiseke Km 2.5, Bigbite Michungwani Km 1.3, Nyasaka Madukani (Jabal hilali - Nyasaka Sokoni) Km 1.1, Mkudi Km 0.25, Ibungilo Km 0.8, Majengo Mapya ( Lumala Sokoni - Kiseke Sec) Km 1.31



Muonekano la daraja la waenda kwa miguu maarufu kama daraja la Furahisha kama linavyoonekana.



Barabara ya njia nne kutoka Makongoro hadi Airport kama inavoonekana eneo la Selrman Nasoro Kata ya Ibungiro.



Barabara ya Mihama - Ibanda ziwani Km 1.30 inavyoonekana, matengenezo bado yanaendelea.

**VIVUKO:** Moja za ahadi ya katika ilani ya uchaguzi Ibara ya 39 (h) (i) ilikuwa ni kuimarisha usafiri majini katika ziwa Victoria. Tunamshukuru sana Mhe Rais kwa kuridhia utoaji wa fedha kiasi cha T**shs. 2,700,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa kivuko cha Kayenze – Baze ikiwa ni hadi iliyotolewa na Mbunge wa Jimbo Dkt. Angeline S.L.Mabula (Mb) wakati akiomba ridhaa kwa wananchi. Ahadi hiyo imetekelezwa kwa **asilimia 100%** na kupewa jina la **MV. ILEMELA.**




Kivuko cha Kayenze – Base maarufu kama MV Ilemela kilichoanza kazi rasmi 19.4.2020, nauli ikiwa na Sh. 1,000 tu, kina uwezo wa kubeba watu 200 na Magari madogo madogo 10.




**Baadhi ya viongozi walioshiriki katika uzinduzi wa safari ya kivuko ka mara ya kwanza kutoka Kayenze kwenda Baze 19.4.2020. Kutoka kushoto ni Meneja wa TEMESA Mkoa wa Mwanza Eng Karonda,Meya wa Manispaa ya Ilemela Mhe Renetus Mulunga, Mtendaji Mkuu wa TEMESA Eng Masele, Mbunge wa Jimbo Dkt Angeline S.L.Mabula, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Wakili Msomi Paul John Wanga OCS wa kituo cha Polisi cha Kayenze**




**Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela Ndugu Paul John Wanga akitoa neon kwa wananchi waliofika kushuhudia safari ya kwanza ya MV Ilemela toka Kayenze kuelekea Baze.**




**Mbunge wa Jimbo Dkt Mabla akiteta jambo na Mtendaji mkuu wa TEMESA kaba ya shughuli ya uzinduzi wa safari ya kivuko MV Ilemela kuanza kazi**



Mtendaji Mkuu wa TEMESA Eng. Masele akitoa neon kwa wananchi waliofika kuhudhulia uzinduzi wa safari za Kivuko cha Kayenze Baze 19.4.2020.

**MIRADI YA KIMKAKATI INAYOENDELEA KUJENGWA KATIKA MANISPAA YA ILEMELA.**

Manispaa ya ilemela ni moja ya Halmashauri ambayo imepewa kipaumbele katika ujenzi wa miradi ya kimkakati ili kukuza uchumi wa nchi, kupitia miundombinu mbalimbali kama vile:

- Upanuzi wa uwanja wa ndege, ambao mpaka sasa njia ya ndege imekamilika, ujenzi wa jumba la mizigo umekamilika, Jendo la kuongozea ndege limekamilika na Rada pia imejengwa na kukamilika
- Ujenzi wa jumba la wasafiri unaendelea na tayari Waziri Mkuu Kasimu Majaliwa Majaliwa aliweka jiwe la msingi tarehe....
- Ujenze wa stand mpya ya Nyamhongolo unaendelea Mradi utakaotumia takribani Tshs Bilion 28 na utakamilika baada ya miezi 18 .
- Ujenzi wa barabara ya lami Km 5 yenye njia nne umekamilika



Jengo la kuhifadhia mizigo katika uwanja wa ndege wa Mwanza limekamilika

Kama linavyoonekana kwa mbele.



Archtect Benno wa kampuni ya OGM ya Dar es salaam akitoa maelezo kwa waziri mkuu Mhe Kasim Majaliwa Majaliwa wakati wa uwekaji Jiwe la msingi katika jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Mwanza




Uwekaji wa Jiwe la msingi katika Jendo la Abiria katika uwanja wa Ndege wa Mwanza.



Jengo la abiria katika standi ya mabus Nyamhongolo ikiendelea kujegwa



### 3.11 Sekta ya Utawala na Raslimali Watu

(i) **Idadi ya Watumishi**

Kwa mujibu wa Ikama iliyoidhinishwa, Halmashauri ina mahitaji ya Watumishi wa sekta zote 3,680, waliopo ni 3,275 na upungufu 405. Pamoja na serikali kuleta watumishi wapya 19 katika kada za Afya na elimu, bado kuna upungufu uliochangiwa na watumishi 96 kukumbwa na tatizo la vyeti vya kughushi katika zoezi la uhakiki wa Watumishi uliofanyika kote Nchini.

(ii) **Uhakiki wa Watumishi**

Halmashauri iliitikia agizo la Serikali la kufanya uhakiki wa watumishi wa Umma ambapo jumla ya Watumishi 2,988 wamehakikiwa. Watumishi 96 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi na Watumishi 24 vyeti vyao vimewasilishwa Baraza la mitihani kwa ajili ya uhakiki na majibu hayajaletwa.

(iii) **Upandishwaji wa madaraja kwa watumishi**

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri iliidhinishiwa ikama ya kupandisha madaraja watumishi 1475, kubadilisha vyeo watumishi 18 pamoja na ajira mpya ya watumishi 208. Hadi sasa jumla ya watumishi 1026 wamepandishwa madaraja na watumishi 988 wamerekebishiwa mishahara yao.

(iv) **Ujenzi wa Jengo la Utawala Makao Makuu ya Halmashauri**

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilipokea fedha jumla ya **Tshs. 1,150,000,000** ikiwa **Tshs 750,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na **Tshs. 400,000,000** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Makao Mkuu ya Halmashauri. Baada ya mapokezi ya Fedha hizo, kazi ya ujenzi wa Ofisi ilianza kupitia kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa mkataba wenye thamani ya T**sh 3,833,822,825.45** ambapo hadi sasa ujenzi uko hatua ya asilimia 38. Hadi sasa kiasi cha **Tshs. 1,196,793,934.50** kimelipwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania kama malipo ya awali. Kulingana na gharama za ujenzi huo yaani **Tshs 3,833,822,825.45,** Halmashauri inapungukiwa kiasi cha **Tshs 2,683,822,825.45** ili kukamilisha ujenzi huo. Hivyo, Halmashauri inasubiri kupatiwa kiasi cha fedha kilichobaki ili kuweza kukamilisha jengo hilo kwa kuwa kwa sasa mkandarasi amesimama kazi kutokana na kukosa fedha.

### 3.*12 Hali ya Umeme Wilayani.*

Wilaya ya Ilemela, KI – TANESCO inahudumiwa na ofisi za Mwanza Mjini, Ilemela na Nyakato. Wilaya inapokea umeme wa Grid kupitia kituo cha Nyakato na vituo vya kusambaza viwili Nyasaka na Sabasaba. Upatikanaji wa umeme katika wilaya ya Ilemela ni wa kuridhisha na maboresho ya miundombinu ya usambazaji inaendelea ili kuondoa tatizo la ukatikaji wa umeme kutokana na hitilafu za hapa na pale zitokanazo na uchakavu wa miundombinu.

#### 3.12.1 Miradi ya Umeme iliyotekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2015/16 hadi 2019/2020

**Miradi mipya (New Extension Projects)**

Miradi ya kupeleka umeme *Kangae Makaburini, Buswelu Stadium, Bujingwa Sokoni,* Miradi hii iligharimu jumla ya Shilingi **132,835,860.00**

**Miradi ya Uboreshaji:** Miradi ya kuboresha umeme *Buswelu Kati,* Miradi hii iligharimu Shilingi **76,678,902.00**

**Miradi mipya (New Extension Projects)**: Mradi wa kupeleka umeme Magaka, Nyamhongolo Juu, Busenga, Masanza karibu na jengo la CCM, Miradi hii iligharimu Shilingi **439,769,967.00**

**Miradi ya kuboresha umeme (2016/17):** Mradi wa kuboresha umeme MECCO – Nundu, Mradi hii iligharimu Shilingi **30,975,66.14**

**Miradi mipya (New Extension Projects) (2017/18)**

Mradi wa kupeleka umeme Kigala Buswelu, Bujingwa block B karibu na Lagos Hotel Miradi hii iligharimu ya jumla ya Shilingi **178,674,705.69**.

**Miradi ya uboreshaji wa umeme (Voltage Improvement)**

Mradi wa kuboresha umeme wa Mahango, Mradi iligharimu jumla ya **Tshs.70,865,097.00**

**Miradi mipya (New Extension projects) 2018/19**

Mradi wa kupeleka umeme Buhyila, Bupumula, Nyambiti na Nyamge. Miradi hii iligharimu ya jumla ya Shilingi **241,313,360.00**

**Miradi ya uboreshaji wa umeme (Voltage Improvement)**

Mradi wa kuboresha umeme kata ya Buswelu na Kahama kwa kujenga laini ya msongo kilovoti 11 umbali wa kilomita 5 (Nyasaka hadi Buhyila). Mradi wa kuboresha umeme wa National – Nyakato. Miradi iligharimu jumla ya Shilingi **232,687,574.18**

**Miradi mipya (New Extension Projects) 2019/2020**

Mradi wa kupeleka umeme *Masanza A & B (Buteja), Mtaa wa Isela & Welunya, mtaa wa Kahama Kati, Mtaa wa Kadinda, Mtaa wa Mwashosha, Mtaa wa Bujingwa, Mtaa wa Bulola, Mtaa wa Nyamadoke & Iwelyashinga, Mtaa wa Kashishi, Mtaa wa Ilamba B, Mtaa wa Ibanda Busisi na Mtaa wa Kirumba Bujumbura.* Miradi hii iligharimu ya jumla ya Shilingi **1,223,680,793.85**. Miradi hii bado inaendelea ikiwa ni Zaidi ya Asilimia 50 katika utekelezaji.

**Miradi ya uboreshaji wa umeme (Voltage Improvement)**

Mradi wa kuboresha umeme wa *Mtaa wa Buswelu A*. Miradi iligharimu jumla ya Shilingi **55,916,611.43** Mradi huu inaendelea katika mwaka wa fedha **2019/20.**





**3.12.2 MIRADI YA REA AWAMU YA TATU MZUNGUKO WA 1**

**Utekelezaji wa Mradi wa REA awamu III mzunguko wa I**

Tunamshukuru sana Mhe Rais Dkt J.P.J.Magufuli kwa kuridhia maeneo ya mijini yenye sura ya vijiji yapewe umeme wa REA. Iliemela kwa kuwa Manispaa hatukustahili kupata umeme wa REA lakini tumepata kutokana na Mhe Rais kujali wanyonge. Mradi wa umeme REA III awamu ya tatu mzunguko wa kwanza katika wilaya ya Ilemela umetekelezwa katika mitaa/vijiji 8 *(Semba, Buganda, Lwashi, Igalagala, Lutongo, Kabusungu, Imalang'ombe na Iponyabugali).*

Mradi bado unaendelea na upo katika hatua za mwisho kukamilika kwa Vijiji/ Mitaa 7 isipokuwa *Imalang'ombe* ambayo inaanza mwezi huu wa Mei 2020. Naendelea kumshukuru sana Mhe Rais mpaka sasa Wilaya imepata umeme wa REA katika mitaa 8 kati ya 56 iliyoko katika maeneo yanayofanana na Vijiji yamefikiwa umeme.

### 3.13 Sekta ya Kilimo na Hali ya chakula Wilayani

#### 3.13.1 Eneo la Kilimo, Mazao na Hali ya Hewa

Eneo linalofaa kwa kilimo katika Wilaya ya Ilemela ni hekta 11,074. Hadi sasa eneo linalolimwa ni hekta 5,369 sawa na asilimia 48 ya eneo lote. Mazao yanayolimwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni pamoja na; Mpunga, Mahindi, Mihogo, Mtama, Maharage, Kunde na mazao ya bustani. Wakulima wengi wanapata kipato chao kutokana na kilimo cha bustani ambacho kinachukua karibu hekta 37. Shughuli za kilimo zinategemea mvua za msimu na kuna misimu miwili ya mvua ambayo ni; Vuli (Oktoba hadi Desemba) na Masika (Januari hadi Mei).

#### 3.13.1 Utekezaji wa shughuli za Kilimo

Hali ya Kilimo cha mazao ya chakula kwa Msimu huu si ya kuridhisha kutokana na Uhaba wa mvua. Kipindi cha vuli ambacho huanza mwezi *Oktoba hadi Desemba* kiliambatana na mvua zilizonyesha vizuri kiasi kwamba Wakulima waliolima mazao makuu hasa ya Mahindi kwa kipindi hicho wamefanikiwa kuvuna. Kipindi cha Masika huanzia *Januari hadi Mei* na kimekuwa kipindi kigumu kwa Wakulima kwani hakuna mvua zilizonyesha na kusababisha utekelezaji wa Malengo ya Kilimo kuwa chini sana ambapo kati ya hekta 668 za Mahindi zilizotarajiwa kulimwa ni hekta 195 tu zilizolimwa toka msimu wa kilimo uanze.

**Bei za bidhaa mbalimbali hadi kuishia mwezi March 2020**

Bei ya sukari imekuwa na changamoto kubwa kila mwaka hasa kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani, bei imekuwa kati ya 2,500 hadi shs 4,000 kwa kilo. Tunaishukuru sana Serikali imekuwa ikiingilia kati kila wafanyabiashara wanapopandisha bei ya sukari. Bei ya Sembe/unga Tshs. 900/= hadi 1000/= kwa kilo. Wafanya biashara wanashuriwa kuleta mahindi kwa wingi ili bei ya soko la unga ishuke ili kumlinda mlaji. Bei ya mafuta ya kupikia Tshs. 2,500/= hadi 4,000 kwa lita Upatikanaji wake ni mzuri.



Wanafunzi waliokuwa wakifundishwa Ujenzi wa kitalu nyumba na kilimo Cha kisasa walifanya kazi kwa vitendo





Picha ya kitalu nyumba kilichopo kata ya Sangabuye jimbo la Ilemela



Picha ya pamoja Kati ya maafisa ugani wa kata zote za Jimbo la Ilemela na wanafunzi waliokuwa wakisomea Ujenzi wa kitalu nyumba na kilimo Cha kisasa kwa ufadhili wa ofisi ya Waziri mkuu kazi, vijana, ajira na walemavu

### 3.14. Sekta ya mifugo na Uvuvi

#### 3.14.1 Sekta ya Mifugo

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ina wafugaji wanaokadiriwa kufika takribani elfu saba kwa mujibu ya sensa ya kilimo na mifugo ya mwaka 2008. Ufugaji wa ndani unatumika zaidi kwenye kata zilizopo maeneo ya mjini kama vile *kata ya Kirumba, Kitangiri, Nyamanoro, Ibungilo, Kawekamo, Pasiansi, Ilemela, Kiseke, Buswelu, Kahama, Nyakato, Buzuruga, Mecco na Nyasaka,* ufugaji huu huhusisha zaidi Ng'ombe na Kuku wa kisasa. Kwa maeneo ya pembezoni mwa mji kama vile Pamoja na ufugaji huo kumekuwa na changamoto kwa wafugaji kutakiwa kuondoa mifugo yao, ama kuwa na ufugaj wa zero grazing kutokana na ukweli kwamba ufugaji huria hauruhusiwi katika maeneo ya mijini. Wafugaji wameshauriwa kupunguza mifugo yao ili waweze kufuga kwa mtindo wa zero grazing. Manispaa ya Ilemela Kitengo cha mifugo kina jumla ya maafisa mifugo 15 kati ya 19 wanaotakiwa hivyo kuna upungufu wa watumishi 4, maafisa mifugo wasaidizi walioko ni 12 kati ya 19 wanaotakiwa, hivyo kufanya kata 7 kukosa wataalam wa mifugo. Mbali na upungufu huo huduma za ushauri na matibabu zimeendelea kutolewa kwa wananchi kama kawaida kwa kutumia wataalamu waliopo.

**Idadi ya Mifugo:** Kwa mujibu wa sensa ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 2008, Halmashauri ina jumla ya Ng'ombe 7148 wa asili na kisasa, Mbuzi 3977, Kondoo 653, Punda 75, Nguruwe 7634, Kuku 7634 na Mbwa 919.

**Huduma za Ugani katika Halmashauri**

Huduma za ugani zimeendelea kutolewa katika Halmashauri kwa kushirikiana na taasisi binafsi kama ifuatavyo**:-**

i. Kuelemisha wananchi kuachana na ufugaji huria usio na tija na kufuga kisasa.

ii. Kutoa huduma za matibabu na chanjo dhidi ya magonjwa hatarishi kwa mifugo na afya ya Jamii.

iii. Kusimamia shughuli za uogeshaji mifugo kwa njia ya pump za mikono ili kudhibiti magonjwa yaenezwayo na kupe

iv. Elimu ya uanzishwaji wa mashamba darasa ya malisho na kuwashawishi wafugaji kujiunga katika vikundi ili waweze kusajiliwa na kutambulika ili kuwarahisishia katika upatikanaji wa mikopo

**Zoezi la Chapa:** Jumla ya ng'ombe 13,626 na punda 192 walipigwa chapa hadi kufikia tarehe 31/03/2019. Zoezi hili lilihusisha ng'ombe wa asili na punda wenye umri wa kuanzia miezi 6 na kuendelea ambapo utekelezaji umefikia asilimia 311.16. Hata hivyo zoezi hili ni endelevu na vifaa vimesambazwa kwenye kila kata hili kuweza kuendelea kuitambua mifugo pindi inapofikisha umri wa kupigwa chapa. Changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi ni kama ifuatavyo:-

i. Kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya Wenyeviti wa Mitaa wengi wao wakidai posho na wengine kutotoa taarifa kwa wananchi kushindwa kuleta mifugo

ii. Wafugaji kutokutoa takwimu halisi za mifugo waliyonayo hivyo kufanya kazi kuwa ngumu kwa kuanza kuhesabu ng'ombe mmoja hadi mwingine.

iii. Maeneo mengi kutokuwa na miundo mbinu mfano kisiwa cha Bezi iliyopelekea zoezi la upigaji chapa kuwa gumu.

iv. Baadhi ya wafugaji kuingilia/kuzuia maafisa wasitekeleze majukumu yao hali iliyopelekea kuita polisi inapobidi.

### 3.14.2 Uvuvi

Wilaya ya Ilemela ina jumla ya kilometa za mraba 1,080 kati ya hizo nchi kavu ni kilometa za mraba 252.7 eneo la maji ni kilo mite za mraba 857.3 tuna mialo kumi na tano (15) kati ya hiyo mialo mitatu (3) ni mialo teule ambayo hupokea na kusafirisha samaki kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Mialo hiyo ni Kayenze (kata ya Sangabuye), New Igombe (kata ya Bugogwa) na Mihama (kata ya Kitangiri).

Aidha Wilaya ina jumla ya vikundi vya ulinzi shirikishi wa rasilimali ya uvuvi (BMUs) 15 vilizosajiriwa kwa mujibu wa sheria ambazo ni; Bezi kisiwani, Tefu kisiwani na Kayenze (Kata ya Kayenze), Igalagala na Lugwigo (Kata ya Sangabuye), Makobe kisiwani, New Igombe, Old Igombe, Kabangaja na Kibandani (Kata ya Bugogwa), Butuja (Kata ya Ilemela), Bwiru (Kata ya Pasiansi), Mihama (Kata ya Kitangiri) na Kigoto (kata ya Kirumba). Kitengo cha Uvuvi Manispaa ya Ilemela kinaendelea na majukumu yake ya utekelezaji wa sheria za uvuvi Na. 22 za mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2009 kwa Kutoa ushauri na Elimu juu ya uvuvi endelevu, Kufanya doria zinazolenga kudhibiti uvuvi haramu, Ushauri wa kitaalamu juu ya ufugaji wa samaki wa kwenye mabwawa na wa vizimba, Kusajili vyombo vya uvuvi na kutoa leseni za uvuvi, Kusimamia na kuvilea vikundi shirikishi vya Ulinzi wa rasilimali za uvuvi (BMU) na Kusimamia Soko la Kimataifa la samaki mwaloni Kirumba. Sekta ya Uvuvi inatoa mchango mkubwa katika uchumi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kuwapatia wananchi ajira, lishe bora na kipato. Kwa mujibu wa Sensa ya uvuvi ya mwaka 2016, Manispaa ya Ilemela ina jumla ya wavuvi wa kudumu 5137. Wavuvi hao wanatumia vyombo vya uvuvi vipatavyo 1436. Aidha, wananchi wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 50,000 wanajishughulisha na kujikimu kutokana na shughuli mbalimbali za uvuvi kama vile utengenezaji wa mitumbwi, uchakataji wa samaki, biashara ya samaki, ukarabati wa zana za uvuvi, uuzaji wa vifaa vya uvuvi, usafirishaji na uchukuzi wa mazao ya uvuvi. Manispaa ya Ilemela inajipatia mapato yatokanayo na makusanyo ya ushuru wa samaki na mazao yake na leseni za vyombo vya uvuvi na wavuvi. Katika mwaka wa fedha **2019/2020** hadi kufikia mwez Desemba Halmashauri iliweza kukusanya kiasi cha **Tshs 555,951,735/=** kutoka katika sekta ya uvuvi.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe Abdallah Ulega akipima samaki kwa rula ili kujiridhisha kama samaki huyo anakidhi viwango.

**SOKO LA KIMATAIFA LA SAMAKI MWALONI, KIRUMBA.**

Soko la Mwaloni Kirumba ni soko la kimataifa linaloshughulika kwa kiasi kikubwa na biashara ya uuzaji na ununuaji wa mazao ya Uvuvi. Soko hili hupokea samaki na mazao yake kutoka ndani ya Ziwa Victoria kama vile dagaa, samaki za maji baridi na mazao yake, furu na konokono. Soko hili ambalo huhudumia watu zaidi ya elfu tatu kwa siku wakiwemo wafanyabiashara kutoka nchi jirani hususani Congo, Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya, Zimbabwe, Malawi na Jamhuri ya Sudani Kusini. Pia soko hili hulisha mikoa ya ndani ya nchi hii na wateja husafirisha kwa kutumia vibali maalumu vilivyowekwa kutokana na Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 na 2015. Mbali na mazao ya uvuvi pia soko hili hushughulika na uuzaji na ununuzi wa mazao ya kilimo (mahindi, mihogo, ndizi n.k), baadhi ya zana za uvuvi (makasia, maboya ya taa za kuvulia dagaa (kismai) na chakula cha mifugo.

**Hali ya Soko na Mapato yatokanayo na mauzo ya samaki.**

Soko la Mwaloni limegawanyika katika sehemu kuu nne ambazo ni Sehemu ya biashara ya chakula (mama lishe), Sehemu ya uuzaji wa mazao ya misitu na baadhi ya zana za uvuvi (kuni, mkaa, kismai, kasia, mikeka), Sehemu ya meza za kuuzia dagaa/mazao ya uvuvi ambapo kwa sasa zipo meza 103 na Sehemu ya uchakataji wa mazao ya uvuvi kutoka viwandani. Kutokana na maboresho makubwa yaliyofanyika kwa kujenga mizani katika kitengo cha mazao ya samaki, mapato yameongezeka sana kutoka **Shs 30,000,000** kwa mwezi ha kufikia zaidi ya **Shs 100,000,000** . Na kwa mapato yatokanayo na mauzo ya samaki ncje ya nchi yameongeeka kutoka **Shs 80,000,000** kwa mwezi hadi kufikia **Shs 400,000,000** kwa mwezi. kwa Maeneo yote hayo hufanyiwa mchakato wa zabuni kutokana na Sheria zilizopo ili kuhakikisha kuwa serikali inakusanya mapato yake halisi. Shughuli za usafi katika soko hili hufanywa na wazabuni ambapo hali ya usafi inaridhisha. Kwa upande wa meza za kuuzia mazao ya uvuvi kwa sasa zinamilikiwa kihalali na wafanyabiashara walioshinda zabuni iliyofanyika Julai, 2018. Pia, eneo la uchakataji wa mabaki ya samaki (fish by-products) limegawanyika katika sehemu za kupokelea na kuoshea mabaki ya samaki (receiving and washing), sehemu ya uchakataji (salting, dripping) na sehemu ya kukaushia kwenye chanja (sun drying).



Lori likiwa limepakia shehena ya Samaki toka soko la kimataifa la Samaki Mwalo wa Kirumba likipimwa uzito wa mzigo kabla ya kuanza safari. Makusanyo yameongezeka maradufu baada ya kufungwa kwa mizani hii.

**3.16 Ushirikishwaji wa Jamii na wadau katika Shughuli za Maendeleo**

Nichukue fursa hii kuwashukuru sana wadau mbalimbali wa maendeleo ambao tumeshirikiana nao kwa kipindi chote kuhakikisha kuwa shughuli za maendeleo zinafanyika kwa ufanisi mkubwa. Wananchi wa Ilemela peke yao kwa kipindi cha 2018/2019 na 2019/2020 wamechangia fedha za kitanzania **Shs. 311,043,715.00** na kufanikisha ujenzi wa miundombinu katika Sekta ya Elimu. Kupitia michango ya wananchi na wadau mbalimbali ambao walichangia mifuko ya sementi, Mabati, Madawati, Ndoo za rangi, Chokaa n.k, shughuli nyingi za maendeleo zimefanyika Jimboni kwa ufanisi mkubwa na kupunguza changamoto ya miundombinu Jimboni.

Michango ya wananchi Kata kwa Kata ni kama inavyoonesha katika jedwali hapa chini:

| **S/NO** | **JINA LA KATA** | **MAKUSANYO 2019** | **MAKUSANYO 2020** | **JUMLA KUU** Tshs. |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KISEKE | 44,101,600.00 | 12,605,300.00 | 56,706,900.00 |
| 2 | BUSWELU | 19,025,000.00 | 14,883,500.00 | 33,908,500.00 |
| 3 | NYAMHONGOLO | 11,072,500.00 | 12,225,000.00 | 23,297,500.00 |
| 4 | KIRUMBA | 15,304,000.00 | 7,111,500.00 | 22,415,500.00 |
| 5 | MECCO | 17,499,400.00 | 3,206,400.00 | 20,705,800.00 |
| 6 | SHIBULA | 13,218,000.00 | 6,057,000.00 | 19,275,000.00 |
| 7 | BUGOGWA | 16,813,100.00 | 1,440,000.00 | 18,253,100.00 |
| 8 | NYAKATO | 14978,500.00 | 2,393,000.00 | 17,371,500.00 |
| 9 | PASIASI | 9,640,000.00 | 6,446,000.00 | 16,086,000.00 |
| 10 | NYASAKA | 8,824,500.00 | 5,242,500.00 | 14,067,000.00 |
| 11 | IBUNGILO | 9,192,000.00 | 3,016,700.00 | 12,208,700.00 |
| 12 | ILEMELA | 7,478,300.00 | 4,394,215.00 | 11,872,515.00 |
| 13 | NYAMANORO | 9,046,600.00 | 2,329,000.00 | 11,375,600.00 |
| 14 | KAWEKAMO | 8,157,300.00 | 1,944,000 | 10,101,300.00 |
| 15 | KAYENZE | 4,527,500.00 | 3,819,000 | 8,346,500.00 |
| 16 | KITANGIRI | 2,920,500.00 | 3,641,000 | 6,561,500.00 |
| 17 | BUZURUGA | 2,344,000.00 | 627,000 | 2,971,000.00 |
| 18 | SANGABUYE | 2,418,200.00 | 375,600 | 2,793,800.00 |
| 19 | KAHAMA | 2,060,000.00 | 666,000 | 2,726,000.00 |
| **JUMLA KUU** | | **218,621,000.00** | **92,422,715.00** | **311,043,715.00** |

**Ushiriki wa wadau katika shughuli za maendeleo**

Mafanikio niliyoyataja katika Sekta mbalimbali hasa katika suala zima la miundombinu, kuna mchango mkubwa sana toka kwa wadau wa maendeleo kama ifuatavyo: BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, Taasisi ya ANGELINE FOUNDATION, MWANZA HUDUMA, PEPSI CO Ltd, SERENGETI BREWERIES, KILIMANJARO SEMENT, TWIGA SEMENT, UBALOZI WA CHINA, NHC, MWANZA COSMOPOLITAN, LAPF, PSPF, NSSF, CRDB BANK, AZANIA BENKI, BENKI YA NMB, DTB BANK, KCB BANK TANZANIA LTD, NAKIETE PHARMACY, NAKOROI LTD, WAENDESHA BODABODA,




Moja ya wadau wa maendeleo Benki ya AZANIA waliochangia mifuko 100 ya sementi mapema mwezi Mei, 2020 na wameahidi kuendelea kushirikiana nasi katika shughuli za maendeleo.




Katibu wa Mbunge Ndugu Kazungu Idebe akipokea sement toka kwa Meneja wa AZANIA Benki tawi la Mwaloni Ndugu SASA kwaniaba ya mbunge wa Jimbo Dkt. Angeline S.L.Mabula (Mb).

Aidha, nawashukuru sana Baraza la Madiwani la Manispaa ya Ilemela chini ya Meya mahiri Mhe Renatus Mulunga, Watumishi wote wa Halmashauri wakiongozwa na Waliki msomi Ndugu John Wanga bila kuwasahau Viongozi wote wa Madhehebu ya dini, na Chama changu cha Mapinduzi chama kilichonipa dhamana ya kuwa Bungeni, kwa ushirikiano wao mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

**4.0 Changamoto zinazoikabili Wilaya**

Pamoja na mafanikio yote yaliyofikiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, bado kuna chamgamoto mbalimbali zinazolikabili Jimbo la Ilemela kwa maana ya Manispaa kama ifuatavyo: Tangu kuanzishwa kwa Wilaya mwaka 2002 na Halmashauri ya Manispaa mwaka 2012 wilaya inakabiliwa na changamoto zifuatazo**:-**

1. Upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali kulingana mahitaji hususani katika sekta ya afya, watendaji wa mitaa na walimu wa masomo sayansi.

2. Mwitikio mdogo wa jamii kujiunga na mpango wa Tiba kwa kadi, na Bima iliyoboreshwa.

3. Miundombinu mibovu ya barabara na hivyo kusababisha adha na usumbufu mkubwa kwa wananchi. Aidha bajeti ndogo wanayotengewa TARURA nayo inachangia

4. Fidia ya ardhi kwa maeneo ya wananchi yaliyotwaliwa kwa ajili ya shughuli za umma kuanzia mwaka 2006 kwa ajili ya matumizi ya Umma hususani ujenzi wa Shule za Sekondari za Kata.

**5.0 Mikakati ya Wilaya kukabiliana na changamoto**

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, Wilaya inaendelea na mikakati mbalimbali kukabiliana na changamoto zilizopo kama ilivyooneshwa hapa chini:-

1. Kuiomba Serikali Kuu kuidhinisha nafasi za kuajiri watumishi hususan wa sekta za Afya, Utawala na Walimu wa masomo ya sayansi.

2. Kutenga fedha katika bajeti na kushirikisha jamii katika kuboresha miundombinu ya kutolea huduma katika sekta za Afya, Elimu, Maji, Barabara na Utawala

3. Kuendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na mpango wa Tiba kwa kadi.

4. Kutenga fedha katika bajeti ili kulipa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Serikali kwa ajili ya shughuli za umma.

Moja ya ziara za kazi Jimboni, katika picha ni vijana wa bodo-boda Kata ya Kayenze wakitoa kero zao kwa mbunge wao.





**Mbunge wa Jimbo akipata Kahawa katika moja ya vijiwe maarufa vya muuza Kahawa Kata Kayenze alipokuwa katika ziara kutembelea Jimbo.**



## 6.0 UJENZI WA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE

Pamoja na kuwa Wilaya ya Ilemela bado ni wilaya changa, takribani miaka 8 tu tangu itangazwe kuwa Halmashauri, kichama wilaya ilianza 2003, tangu wakati huo haijawa na miradi mingi kuifanya ijitegemee kwa shughuli mbalimbali za maendeleo. Aidha shughuli nyingi za chama zimekuwa zikiendeshwa kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wawakilishi wa wananchi Mbunge na Madiwani. Kumekuwepo na ushirikiano mzuri baina ofisi ya mbunge, ofisi ya chama Wilaya na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, hakika sina budi kuwashukuru Watendaji wote wa Chama na Serikali niliofanya nao kazi kwa nyakati tofauti nikianzia na Ndg Maulid Acheni, Ndg Michael Chonya na hatimaye Bi Aziza Simbula ambae tunaendelea nae, kwa ushirikiano wao kwa wakati wote.

Aidha shughuli nyingi za kukijenga chama zimekuwa ni za kujitolea kwa wanachama na viongozi wake. Kama mwakilishi, nimekuwa nikijitolea kwa hali na mali kuhakikisha kuwa shughuli za chama hazikwami hasa pale zinapohitaji raslimali fedha. Mfano; Matengenezo ya Gari la Chama, Ununuzi wa mafuta ya gari, Gharama za Vikao mbalimbali, Sare za chama kwa Jumuia za chama hasa wakati wa mikutano na shughuli mbalimbali za chama, jambo ambalo naona fahari kuhudumia kama mwanachama lakini pia kama kiongozi.




Mbunge wa Jimbo la Ilemela akikabidhi taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi kwa Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Bashiru Ally Kakurwa siku moja kabla ya kusoma taarifa mbele ya wajumbe wa Mkutano mkuu wa Jimbo



Ziara ya katibu mkuu ndgu Bashiru Ally alipotembelea na kukagua ujenzi wa Jengo la Ofisi ya CCM



Ziara ya Mbunge kuongea na halmashauri Kuu ya kata ya Buswelu



Kikundi cha amani Kilimihewa kilichotengeneza kitenge na kikavaliwa wakati wa sherehe za uhuru tarehe 9.12. 2019 kwa ushauli wa Mbunge wa Jimbo





Baadhi ya Viongozi walioshiriki Pamoja na Katibu Mkuu wa CCM Ndg Bashiru Ally wakati wa kusuma taarifa ya Utekelezaji 2015 - 2019




Viongozi mbalimbali walioambatana na Katibu Mkuu Ndg Bashiru Ally Kakurwa ambae alikuwa mgeni rasmi wakati wa uwasilishaji utekelezaji wa ilani ya uchaguzi 3.8.2019 Uwanja wa CCM Kirumba



Watoto wa shule ya msingi Gedeli wakitumbuiza.





Baadhi ya wajumbe wa mkutano mkuu wa Jimbo uliofanyika 3.8.2019 wakimsikiliza Mbunge akiwasilisha utekeleza wa Ilani



Aliyekuwa Katibu wa CCM wilaya ya Ilemela ambae kwasasa ni Katibu wa CCM Mkoa wa Kagera Michawl Chonya akitoa neno kwa wajumbe wa mkutano mkuu 3.8.2019






Kikundi cha ngoma cha Chapakazi kutoka Kata ya Nyamhongolo kikitoa burudani wakati wa mkutano



**Akina mama wa Kata ya Ilemela wakiimba shairi wakati wa uwasilishaji Utekelezaji wa ilani 3.8.2019**

Kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia **2015** hadi **2020,** jumla ya fedha **Shs. 131,999,000.00** zimetumika kwa shughuli mbali mbali za chama na jumuiya zake kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini;

### 7.0 MICHANGO YA MBUNGE KUIMARISHA CHAMA NA JUMUIYA ZAKE

| Na | Maelezo | Chama | Jumuiya za chama | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | UWT | WAZAZI | UVCCM |
| 1 | Ununuzi wa Mabati 300 gauge 28 Sh 5,250,000 Ujenzi wa jengo la ofisi la Chama Buswelu Sh. 2,320,000, Service ya Gari la Chama Sh 3,800,000, Ukarabati wa Choo cha ofisi ndogo Sh. 1,200,000 | 12,570,000 | | | |
| 2 | Tairi na mafuta ya gari la chama | 6,500,000 | | | |
| 3 | - Gharama za vikao na mikutano ngazi ya wilaya<br><br>-Gharama za vikao vya Halmashauri kuu za Kata zote 19 | 45,250,000<br><br>25,700,000 | | 2,100,000 | 3,200,000 |
| 4 | Sare za Chama kwenye Jumuiya - Tshirt na, Vitenge | | 3,714,000 | 1,500,000 | 6,750,000 |
| 5 | Katiba za chama | 350,000 | | | |
| 6 | Gharama za semina kwa UWT na Mabalozi | 12,300,000 | 3,900,000 | | |
| 7 | Ununuzi wa bendera 700 za mabalozi | 2,100,000 | | | |
| 8 | Ununuzi wa Shajara kwa ajili ya Ofisi zote za chama ngazi ya Kata Matawi na Jumuiya ngazi ya Wilaya | 1,836,000 | | | |
| 9 | Motisha kwa Kata tatu *Sangabuye, Nyamhongolo na Kahama* zilizofanya vizuri katika uchaguzi mkuu wa Rais, Mbunge na Madiwani, 2015 | 3,200,000 | | | |
| **Jumla** | | **109,806,000** | **7,643,000** | **3,600,000** | **10,950,000** |

**FEDHA ZILIZOTOLEWA NA MBUNGE PAMOJA NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KATIKA HUDUMA MBALIMBALI**

| S/no | KATA | MAELEZO YA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KATA | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Elimu | Afya | Maji | Huduma za Jamii | Uvuvi | Polisi |
| 1 | Kayenze | 26,906,00 | | | 1,920,000 | | |
| 2 | Sangabuye | 15,917,500 | 120,000 | | 1,820,000 | | |
| 3 | Bugogwa | 84,773,485 | 15,000,000 | 4,345,000 | 4,690,000 | 2,500,000 | |
| 4 | Shibula | 26,437,900 | 4,300,000 | 12,457,000 | 3,240,000 | | |
| 5 | Kahama | 40,788,400 | | 4,000,000 | 1,410,000 | | |
| 6 | Buswelu | 65,320,225 | | | 1,060,000 | | |
| 7 | Nyamhongo-lo | 48,612,485 | 3,000,000 | | 560,000 | | 5,000,000 |
| 8 | Nyakato | 27,338,400 | | | 400,000 | | |
| 9 | Mecco | 26,166,400 | | | 390,000 | | |
| 10 | Buzuruga | 16,939,400 | | | 2,390,000 | | |
| 11 | Nyasaka | 22,048,400 | | | 1,330,000 | | |
| 12 | Ilemela | 26,064,400 | 9,000,000 | | 150,000 | | |
| 13 | Nyamanoro | 23,720,800 | | | 580,000 | | |
| 14 | Kawekamo | 21,360,400 | | | 600,000 | | |
| 15 | Pansias | 25,155,700 | | | 1,160,000 | | |
| 16 | Kirumba | 37,080,275 | 5,029,000 | | 840,000 | | |
| 17 | Kitangiri | 14,768,400 | 2,000,000 | | 1,170,000 | | |
| 18 | Ibungiro | 7,000,000 | | | 720,000 | | |
| 19 | Kiseke | 20,000,000 | 7,120,000 | 1,000,000 | 540,000 | | 3,000,000 |
| | **JUMLA** | 537,857,420 | **32,069,000** | **21,802,000** | **24,970,000** | **2,500,000** | **5,000,000** |

## 8.0 TAASISI YA ANGELINE FOUNDATION NA UWEZESHAJI WA JAMII

Taasisi hii imetimiza miaka 4 tangu ilipoanzishwa Machi 2016 na marejeo ya usajiri no 00NGO/R2/000361 ya 10 August 2019 baada ya sheria mpya kuanza kutumika. Awali taasisi ilikuwa na usajili chini ya sheria CAP 212 ya 11 March 2016. Lengo na madhumuni ya kuundwa kwa taasisi hii, ni kurahisisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa jamii, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Tangu kuundwa kwa taasisi hii kazi zifuatazo zimefanyika, kama inavyojionesha katika jedwali lifuatalo;



**Mashine ya tofali iliyonunuliwa Manispaa ni msaada mkubwa katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu, Afya na ofisi za utawala**



**Baadhi ya vijana wakiofurahia kazi yao katika mradi wa tofari**

## MAFANIKIO YA HUDUMA ZA TAASISI YA ANGELINE FOUNDATION KWA KUSHIRIKIANA NA WADAU WA MAENDELEO

| NA | MATUMIZI | FEDHA ZILIZOTU-MIKA | WANUFAIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ununuzi wa vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa Covid 19 unaosababishwa na virus vya Corona Ndoo, Sabuni, Vitakasa mikono na Barakoa | 35,800,000.00 | Taasisi za Dini, Vituo vya Daladala, na waendesha Bodaboda, vituo vya wauza Kahawa, Wenyeviti wote wa Mitaa, Ofisi za Chama Wilaya, Kata na Matawi, na wenyeviti wa Mitaa. |
| 2 | Sadaka iliyotolewa kipindi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani na siku kuu za Eid elftri na Pasaka | 38,850,000.00 | Wajane na watoto yatima, Viongozi wa dini (BAKWATA) ngazi ya Mkoa na Wilaya, Viongozi wa Chama ngazi ya Halmashauri kuu za Kata |
| 3 | Mafunzo ya ujasiliamali kwa vikundi mbalimbali vya Wanawake na Vijana | 17,550,000.00 | Zaidi ya vikundi 627 vimepata mafunzo ya ujasiliamali toka Kata 19 |
| 5 | Kukodi grader na kuweka mafuta kwa ajili ya kazi za uchongaji barabara | 13,717,000.00 | Ujenzi wa miundombinu ya Barabara Km 27.3 katika Kata ya Kahama, Kayenze, Bugogwa na Shibula |
| 6 | Huduma za gari la kwa ajili ya marehemu wetu na rambirambi zilizotolewa | 25,110,000.00 | Kata zote 19 zilipata huduma kwa marehemu wao ikiwa ni huduma ya gari, fedha taslimu za rambirambi au vyakula na maji ya kunywa |
| 7 | Ufyatuaji wa matofali kwa ajili ya matumizi ya kujengea miundombinu ya Afya, Elimu, Utawala na ofisi za Chama | 250,875,000.00 | Kata zote 19 zimenufaika na huduma hii ya tofali katika sekta ya Elimu, Afya, Utawala na Chama |
| 8 | Ugawaji wa mifuko 766 ya sementi katika taasisi mbalimbali, watu binafsi na madhehebu ya dini | 13,405,000.00 | Sementi ilitolewa kwa taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Shule za msingi zikiwemo na shule binafsi, Sekondari, madhehebu ya dini na watu binafsi |
| 9 | Misaada mbalimbali ya elimu kwa wanafunzi 30 wasio na uwezo na wale wa mazingira magumu na wahitaji, ikiwa ni ada na mahitaji ya shule, matibabu n.k | 15,500,000.00 | Jumla ya Kata zote 19 zimenufaika na msaada huo, na wengine wanatoka nje ya jimbo. Kati yao watatu wako vyuo vikuu |
| 10 | Ugawaji wa madawati 1923 ikiwa ni mchango katika shule Jimboni zilizohitaji msaada huo. | 163,445,000.00 | Kata zote 19, zilinufaika na madawati |
| 11 | Ujenzi wa chumba cha Maabara katika kituo cha afya Buzuruga | 15,000,000.00 | Wananchi wakazi wa Kata ya Buzuruga na Kata jirani Nyakato, Mecco, Nyasaka,, Nyamhongoro na wilaya jirani ya Magueneo la Kisesa |
| 12 | Ununuzi wa vifaa vya michezo kwa ajili ya Jimbo Cup, UMISETA, UMITASHUMTA, michezo ya Vilabu mbalimbali na Bonanza la waalimu | 135,570,000.00 | Timu shiriki zote katika mashindano ya Jimbo Cup kwenye kata 19 na Timu za shule katika mashindano ya wilaya na Taifa UMITASHUMTA, UMISETA), na Waalimu wa michezo hiyo |

| NA | MATUMIZI | FEDHA ZILIZOTU-MIKA | WANUFAIKA |
|---|---|---|---|
| 13 | Ada na matumizi ya shule kwa wanafunzi wahitaji | 10,500,000.00 | Wanafunzi 45 katika shule na vyuo mbalimbali waliofika kuomba msaada ofisi ya Mbunge |
| 14 | Ununuzi wa vitabu vya sayansi katika shule 3 za Sekondari (Ibinza, Mihama na Kilimani) | 8,200,000.00 | Wanafunzi kidato cha kwanza hadi cha nne katika shule husika |
| | Total | **753,519,000.00** | |

## MATUMIZI YA MFUKO WA JIMBO 2015 - 2020

| MWAKA | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | FEDHA TUMIKA KISHUGHULI | SHUGHULI ZILIZOFANYIKA |
|---|---|---|---|---|---|
| 2015/16 | 51,398,000.00 | 51,398,000.00 | 53,156,000.00 | 53,156,000.00 | Utengenezaji wa madawati 530 katika shule za msingi. |
| | | | **JUMLA** | **53,156,000.00** | |
| 2016/17 | 51,398,000.00 | 50,029,000.00 | 50,029,000.00 | 5,029,000.00 | Ujenzi wa kivuli cha zahanati Kirumba |
| | | | | 19,650,000.00 | Kuchonga barabara ya Ilalila, Kabusungu, Igumamoyo-Sangabuye sekondari km 8, Kahama,Isela, Masemele-Isesa Km14. |
| | | | | 924,000.00 | Kurejesha fedha serikali kuu iliyozidi |
| | | | | 24,426,000.00 | Kukodi Gari na ununuzi wa mafuta. |
| | | | **JUMLA** | **50,029,000.00** | |
| 2017/18 | 59,726,000.00 | 59,726,000.00 | 56,000,000.00 | 54,000,000.000 | Ufyatuaji wa matofali 67,500 kwa ajili shughuli za maendeleo katika mitaa na Kata za Manispaa kutoka katika Mfuko wa jimbo (Semaul undong group) |
| | | | | 1,000,000.00 | Ujenzi wa kalvati/daraja katika mtaa wa Mecco mashariki |
| | | | | 1,000,000.00 | Ujenzi wa kivuli katika Zahanati ya Nyamhongolo |
| | | | **JUMLA** | **56,000,000.00** | |
| 2018/19 | 60,396,000.00 | 58,396,000.00 | 62,989,410.00 | 11,870,000.00 | Ununu wa mabati kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maabara shule ya Sekondari Kirumba |
| | | | | 5,000,000.00 | Kuwezesha vikundi kiuchumi vya vijana, wanawake na walemavu |
| | | | | 2,475,750.00 | Kufanya ukarabati wa nyumba ya Mwalimu shule ya Msingi Kayenze |
| | | | | 43,548,660.00 | Mradi wa ufyatuaji matofari na gharama za vibarua |
| | | | **JUMLA** | **62,989,410.00** | |
| **2019/20** | 60,396,000.00 | 60,396,000.00 | 60,396,000.00 | 2,500,000.00 | SACCOS ya Wavuvi Igombe |
| | | | | 36,912,000.00 | Miradi ya Kata |
| | | | | 20,984,000.00 | Ununuzi wa mifuko ya Simenti 1220 kwa ajili ya ufyatuaji wa tofari |
| | | | **JUMLA** | **60,396,000.00** | |
| **JUMLA KUU** | **283,314,000.00** | **279,945,000.00** | **282,570,410.00** | **282,570,410.00** | |

## 9.0 MICHANGO MBALIMBALI KATIKA JAMII

Kwa kutambua kuwa jamii inamahitaji mbalimbali na hasa kwa wale wasiokuwa na uwezo au watoto wenye mahitaji katika shule mbalimbali, ofisi ya Mbunge imesaidia katika kugharamia masomo yao, matibabu, mahitaji ya familia n.k. Aidha, kwa kuwa tunashiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile harusi, maafa, au sherehe za kidini n.k. Haya yote yamekuwa yakifanyika kutegemeana na nafasi inayokuwepo kifedha. Mambo machache nitayaainisha hapa kwa yale yanayokumbukwa tu japokuwa huduma ya uchangiaji katika jamii imefanyika kwa mapana zaidi ya kinachoripotiwa hapa. Jumla ya wanafunzi 66 kati yao 32 ni katika shule za sekondari na 29 katika Chuo cha Ufundi Malya na 5 shule za msingi, wamesaidiwa kielemu.

### MCHANGANUO WA FEDHA ZA MFUKO WA JIMBO KWA MWAKA 2020 (MWAKA MMOJA)

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLE-WA | FEDHA TUMIKA |
|---|---|---|---|
| Mwanza huduma ununuzi wa mifuko 1220 ciment ufyatuaji wa tofari | 20,984,000.00 | 20,984,000.00 | 20,984,000.00 |
| Kutoa msaada vikundi vya ushirika wavuvi - Igombe | 2,500,000.00 | 2,500,000.00 | 2,500,000.00 |
| **JUMLA** | **23,484,000.00** | **23,484,000.00** | **23,484,000.00** |
| Ujenzi wa Ofisi ya Mitaa ya Sangabuye Nyafla na Kabusungu | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| **JUMLA** | **2,000,000.00** | **2,000,000.00** | **2,000,000.00** |
| Zahanati ya Ilemela ujenzi wa chumba cha upasuaji | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | |
| Ukarabati wa nyumba ya mtumishi Lukobe | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| **JUMLA** | **4,000,000.00** | **4,000,000.00** | 4,000,000.00 |
| Ujenzi wa vyumba madarasa shule ya Kisundi | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuweka mfumo wa maji shule ya Msingi Mihama | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 |
| Kuwezesha kuweka mfumo wa umeme shule Msingi Buzuruga | | | |
| Kuwezesha kuweka mfumo wa umeme shule Msingi Nyambiti | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 |
| JUMLA | **5,000,000.00** | **5,000,000.00** | **5,000,000.00** |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba 3 vya maabara Angelina Mabula | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madara shule ya sekondari Kisundi | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kuweka mfumo wa umeme Shule ya Sekondari Mwinuko | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Kilimani | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara Shule ya Sekondari Kayenze | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara Shule ya Sekondari Kiloleli | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Nyamanoro | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Ibinza | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Kabuhoro | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara Shule ya Sekondari Nundu | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa matundu ya vyoo Shule ya Sekondari Kangaye | 1,912,000.00 | 1,912,000.00 | 1,912,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Nyasaka | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Kitangiri | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| Kuwezesha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Shibula | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 | 2,000,000.00 |
| JUMLA | **26,912,000.00** | **26,912,000.00** | **26,912,000.00** |
| JUMLA MKUU | **60,396,000.00** | **60,396,000.00** | **60,396,000.00** |

## 10.0 HAMASA, MICHEZO NA UTAMADUNI

Kwa kuzingatia kuwa mimi ni mwanamichezo, suala la michezo ni kipaumbele changu muda wote. Aidha mashindano mbalimbali ya vilabu, wanafunzi na Vijana yamekuwa yakifanyika kwa nyakati tofauti tofauti na ofisi ya mbunge imekuwa ikifadhili michezo hiyo. Mashindano ya Angeline Ilemela Jimbo Cup yalianzishwa rasmi Mwaka 2016, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mbunge wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Mashindano hayo yenye kauli mbiu ya 'MICHEZO NI AJIRA, MRUHUSU MWANAO' yamekuwa yakifanyika ili kuibua vipaji vya wana michezo wanaochipukia ndani ya Jimbo. Hii inatokana na historia ya kuwa na vijana wengi wenye vipaji mbalimbali, na hata imesababisha kutoa wachezaji wengi katika timu kubwa kubwa hapa nchini kama vile club za Yanga, Simba, Azam na nyinginezo wamekuwa wakichukua wachezaji toka Ilemela. Aidha, uanzishwaji wa mashindano haya ilikuwa ni utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuwataka wananchi kushiriki katika michezo. Aidha tumekuwa tukishirikianana taasisi ya Tanzania Football House (TFH) ambayo ni taasisi ya kijamii inayo shughulika na kuinua vipaji vya vijana wanamichezo imekuwa ikishirikiana na taasisi ya "The Angeline Foundation" kwa pamoja wamekuwa wakilea vipaji vya Vijana wanaokaa mashuleni. Mpaka sasa tunao vijana sita ambao wako kambini Bwiru ambao ni Kelvin John mchezaji wa Serengeti boys, Machumu Malagila Youngman, Nassoro Omary Mfaume, Augustion Athanas Chalamba, Adam Ramadhani Mohamed Fumbwe. Kwa sasa Kelvin John amefanikiwa kufanya majalibio ya mpira wa kulipwa nchini Sweden na Africa Kusini.

## 11.0 UJENZI WA VITUO VYA MICHEZO

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa kushirikiana na ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Ilemela sambamba na shirika la kijamii la Mwanza Sports Charity wana malengo yakujenga vituo vya michezo 10 katika maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Ilemela. Kwa kuanzia kituo cha michezo Sabasaba (ILEMELA SPORTS CENTER) ambacho kimejumuisha viwanja vya michezo vya Mpira wa Miguu (kikubwa na kidogo), Uwanja wa mpira wa kikapu (Basketball), Uwanja wa Mpira wa Pete (Netball), Uwanja wa mpira wa wavu (Volleyball) na sehemu ya kukimbilia watu wazima, tayari vinatumika baada ya kukamilika ujenzi wake. Mpaka sasa clubs za TSC Academy, Planet Basketball Academy, Pansias Vollebal na timu zingine wanatumia viwanja hivyo. Aidha shukurani zimwendee *Ndugu Kiziti Isomela Bahati a.k.a SOSHO* amekuwa mstari wa mbele kusimamia michezo mbalimbali katika viwanja hivyo.

Kituo hiki kikikamilika kitagharimu zaidi ya shilingi milioni mia moja na ishirini (120,000,000.00) za kitanzania kwa sasa ujenzi imefikia 95%.




Timu ya watoto wa shule za msingi waliyoshiriki michezo ya UMITASHUMTA





Afisa Elimu wa Elimu ya Msingi Mwl. Busungu akikabidhi zawadi ya kikombe kwa captain wa timu ya walemavu wangozi



Mbunge wa Jimbo Dkt Mabula akiongea na timu zilizoshiriki kombe la Ramadhani 2018 kabla yakukabidhi zawadi kwa washindi wa kombe hilo. Zawadi mbalimbali zilitolewa ikiwemo Ng'ombe, Mbuzi na jezi kwa washindi.

## 12.0 USHIRIKI WA VIKAO

Napenda kumshukuru sana Dkt J.P.J.Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa msaidizi wake katika Wizara ya Ardhi nyumba na maendeleo ya Makazi, nafasi ambayo nimedumu nayo kwa kipindi chote cha miaka 5. Nafasi hii haikuwa kikwazo cha kutoshiriki katika vikao vyote vya Kikatiba kuanzia ngazi ya Tawi, Kata, Wilayani, Mkoani na Taifa kwa ujumla. Naahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa viongozi wangu wote wa Chama kwa ngazi zote.



**Naibu Waziri wa Ardhi Dkt Angelina Mabula akijibu swali bungeni**



**Moja ya vikao vya mwisho kabla ya kuvunjwa bunge 16/06/2020. Nikiwa na manaibu waziri wa Elimu, Maliasili na utalii na Mambo ya nje. Kwa chini ni mawaziri wa Maji, Maliasili na utalii na Habari utamaduni na michezo**



Picha za pamoja za wabunge baada ya Bunge kuahirishwa



Picha ya pamoja na waziri mkuu Mh kasimu Majaliwa Majaliwa baada ya kuahirishwa bunge la 11 la Jamhuri ya muungano wa Tanzania



Manaibu waziri kuanzia kushoto Mhe stella Ikupa - OWM walemavu, Dr Mary Mwanjelwa - OR Utumishi, Mhe Stanalaus Nyongo Dr Ashatu Kijaji - Fedha



Manaibu waziri Mhe Stella Manyanya Viwanda na Biashara, Mhe Subira Mgalu - Nishati, Dr Angeline Mabula - Ardhi



Picha ya pamoja na Chief Whip Mhe Jenister Mhagama.



## 13.0 MAHUSIANO NA JAMII

Namshukuru Mungu kwa namna alivyonijalia kuwa na mahusiano mazuri na jamii inayonizunguka, hasa wananchi ninaowawakilisha. Ofisi ya Mbunge pamoja na taasisi ninayoiongoza imekuwa na mahusiano mazuri sana ndani na nje ya chama ikiwa ni pamoja na jamii ninayoiwakilisha. Kwa kipindi chote cha miaka mitano uhusiano na wananchi ninaowawakilisha umekuwa imara na yameongeza kasi ya maendeleo yanayoonekana Jimboni kwa kuwa sehemu kubwa ya misaada na michango wanayochangia wadau imetumika katika kuweka miundo mbinu katika Sekta ya Elimu, Afya, Utawala, Chama na hata kwa wananchi wakawaida kabisa waliohitaji msaada wa Mbunge. Kwa mahusiano hayohayo nimeweza pia kualika makundi mbalimbali kuja bungeni kujifunza namna shughuli za bunge zinavyoendeshwa wakiwemo, Viongozi wa chama, Madiwani, Wanafunzi, Wanamichezo, Viongozi wa madhehebu ya dini, Wajasiliamali n.k.







Unapokuwa mtumishi wa umma huna budi kujifunza mila za watanzania





## 13.0 ZIARA NA MIKUTANO MBALIMBALI JIMBONI

Kwa kipindi chote cha uwakilishi wangu nimefanya ziara 57 kuongea na Halmashauri kuu zote 19 mara tatu kila kata, Mikutano mikuu ya uwasilishaji utekelezaji wa Ilani mikutano mikuu imefanyika mikutano 2, na taarifa ya tatu umekamilika na itasambazwa kwa wadau wote Jimboni. Aidha ziara za kusikiliza kero na urejeshaji wa utendaji kwa jamii jumla ya mikutano na ziara 309 zimefanyika Jimboni. Vile vile ziara kwa kushirikiana na Mawaziri na Manaibu waziri kadhaa wametembelea Jimboni ama kutatua kero ama kukagua miradi ya maendele iliyo chini ya wizara zao. Mawaziri wote waliotembelea Jimbo kila mmoja ameleta manufaa ndani ya wilaya, Mfano Barabara, Maji, Vituo vya Afya, Ukarabati wa shule za Sekondari, Ujenzi wa Kivuko cha Bezi n.k.



**Picha ya pamoja na viongozi wa kata ya Nyakato wakati wa ziara kuongea na Halmashauri kuu za kata**





**Baadhi ya viongozi ngazi ya wilaya ya Ilemela wakimsubiri Katibu wa NEC - Itikadi na uenezi Ndugu Humphrey Polepole wakati wa maadhimisho ya CCM 2020 mkoani mwanza**

## 14.0 CHANGAMOTO

Changamoto kubwa tunayokumbana nayo katika utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ni;

- Kutokuwepo ama kuchelewa kwa fedha za miradi ya maendeleo na fedha kutokidhi mahitaji na huduma za jamii.
- Upungufu wa watumishi katika ngazi zote unaosababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali.
- Baadhi ya wananchi kupotosha ukweli juu ya ushirikishaji wa jamii katika kuchangia miradi ya maendeleo kwa kigezo kuwa Serikali inatoa kila kitu.
- Migogoro ya ardhi inayosababishwa na kutolipwa fidia kwa wakati, kwa wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa na Serikali kwa shughuli za umma.
- Baadhi ya viongozi wachache kupotosha ukweli juu ya ufumbuzi wa kero katika jamii na hasa migogoro ya ardhi, na hivyo kuchochea migogoro baina ya wananchi na wawakilishi wao.
- Wananchi kutokuwa na subira katika utatuzi wa changamoto zinazowakabili

## MATARAJIO

Kutokana na mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika awamu ya tano katika utekelezaji wa Ilani, na kasi ya Mhe Rais Dkt. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni wazi changamoto zote zinazolikabili Jimbo la Ilemela zitapatiwa ufumbuzi. Aidha mpaka sasa zoezi la kuhakiki wananchi ambao maeneo yao yalitwaliwa na Jeshi miaka ya nyuma limekamilika na malipo yameanza kutolewa eneo la Nyagunguru wamelipwa na Lukobe uhakiki umekamilika wanasubiri malipo. Aidha wakazi wa Polisi Kigoto na wanaendelea kurasimishiwa maeneo yao baada ya Mhe. Rais kuridhia wananchi hao wabaki katika eneo hilo na Polisi wapewe eneo lingine.

## 15.0 SHUKURANI

Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge aidha namshukuru sana Mhe, Dkt John P.J.Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa CCM Taifa, kwa kuniamini kwa kipindi chote kumsaidi katika wadhifa wa Naibu Waziri Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nasema asante sana. Aidha kasi yake katika utendaji imeing'arisha nchi yetu ulimwenguni, kwani Mataifa mengi yamekuwa yakisifia kasi ya mabadiliko ya kiuchumi kwa taifa letu. Mhe Rais amekuwa ni kiongozi mahiri, na mwenye maono ambayo kila uchao Tanzania inang'ara Kimataifa. Aidha niwashukuru sana Wadau wote wa Maendeleo kwa njia moja ama nyingine wamewezesha shughuli za Jimbo kufanyika kwa kiwango kikubwa kabisa, chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Niwashukuru Viongozi wote wa Madhehebu ya dini mbalimbali kwa sala na maombi yao, ambayo yamewezesha amani kuendelea katika nchi yetu na Jimbo kwa ujumla. Nakishukuru sana chama changu cha CCM kuanzia ngazi ya Shina hadi Taifa kwa maelekezo mbalimbali katika utekelezaji wa ilani, na kwa kuisimamia vyema Serikali. Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wananchi wote wa Jimbo la Ilemela kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao, ninaahidi kwao kutowaangusha kwa kuwa Imani huzaa Imani nami nasema kamwe sitawaangusha. Aidha naishukuru Halmashauri yangu ya Manispaa ya Ilemela chini ya Mstahiki Meya Renatus Bahebe Mulunga kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Halmashauri ya Manispaa, Waheshimiwa Madiwani wote, Mkurugenzi wa Manispaa Ndugu Paul Wanga na Watumishi wote wa Halmashauri kwa ushirikiano wao mkubwa ambao umewezesha utekelezaji wa Ilani kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Niwashukuru watendaji wote ofisi ya Mbunge ambayo imegawanyika katika Kanda nne (4) Buswelu, Bugogwa, Kirumba na Nyakato. Nikianza na Katibu wa Mbunge mwanzilishi Comrade Kheri D.James ambae aliweka msingi mzuri katika usimamizi wa shughuli za ofisi ya Mbunge, Mwl Michael Goyele ambae alipokea kijiti na kuendeleza mapambano ya maendeleo katika Jimbo, tatu Ndugu Kazungu Idebe ambaye ndiye Katibu wa Mbunge kwa sasa hakika kasi ya utendaji kazi inaonekana. Mratibu

wa Jimbo Ndg Mpunzi Mbegeje, Ndg Abubakari na Waratibu katika Kanda; Kanda Nyakato ikiongozwa na Ndugu John Makorosho, Kanda ya Kirumba chini ya Ndugu Fatuma Kalori, na Kanda ya Bugogwa chini ya Ndugu Rebecca Yusuph ni ukweli usiopingika kuwa watu hawa wamekuwa kiungo kizuri kati ya Wananchi na ofisi ya Mbunge.

Mwisho nimalizie shukurani zangu japo si kwa umuhimu Familia yangu kwa kunivumilia wakati wote hata pale nilposhindwa kutekeleza majukumu ya familia kwa kubanwa na majukum ya Serikali. Aidha naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kuniunga mkono wakati wote nikifanya kazi za uwakilishi. Pamoja na kupoteza Baba mzazi Mzee Sylvester Lubala, Baba mdogo Mzee Abel Lubala, na Mume wangu mpendwa Ndugu Julius Mabula, ukweli ni kwamba hatuko nao kimwili lakini kiroho tuko pamoja nao. Ninaimani kwa maombezi yao tutaendelea kufanya vyema na kwa kudra ya mwenyezi Mungu ataendelea kutupa ujasiri wakufanya. Naendelea kumuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutuhekimisha sote tutende kazi za jamii kwa moyo thabiti na uadilifu mkubwa.

## 16.0 HITIMISHO

Kasi ya awamu ya tano katika mafanikio yaliyopatikana ni kielelezo tosha cha uchapakazi wa Rais wetu Dkt J.P.J.Magufuli kiasi cha kuakisi utendaji kwa watanzania wote kwa ujumla wao. Aidha usimamizi na ufuatiliaji wa viongozi wa chama katika utekelezaji wa ilani umechangia kuleta maendeleo chanya katika miradi mbalimbali, na hivyo kuhakikisha huduma za msingi za jamii zinapatikana kwa wananchi. Aidha, Serikali ya wilaya itaendelea kusisitiza na kumtaka kila mwananchi mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye kwa bidii na weledi mkubwa ili kuleta tija katika uzalishaji; na kusimamia vyema utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi. Vita dhidi ya Rushwa na ubadhirifu wa mali za umma kila mmoja wetu ashiriki. Aidha kusisitiza suala la uzalendo kwa wananchi na kuwa tayari kushirikiana na wawekezaji katika uwekezaji wa viwanda vitakavyotumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini kwa lengo la kuongeza ajira kwa vijana wetu na kuongeza pato la mwananchi mmoja mmoja na wilaya kwa ujumla, ili nchi iweze kufikia malengo ya vipaumbele vya kitaifa (national priorities). Haya yote yanawezekana kutokana hali ya amani na utulivu iliyopo miongoni mwetu kama Watanzania hususani wana Ilemela.



Taarifa hii imeandaliwa na Ofisi ya Mbunge wa Ilemela kwa kushirikiana na ofisi ya Mchumi wa Manispaa ya Ilemela

**“ JIKINGE WAKINGE NA WENGINE CORONA INADHUHIRIKA, CHUKUA TAHADHARI. ”**



**MH: ANGELINA MABULA**

Naibu waziri wa Ardhi

- Osha mikono yako kwa sabuni ya maji safi yanayo tiririka mara kwa mara.
- Hakikisha unafunika pua na mdomo kwa kitambaa safi au (mask).
- Epuka mikusanyiko au msongamanowa watu.
- Epuka kusalimiana kwa kugusana au kushikana mikono.



**Mhe. Samia Suluhu Hassan,**
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania na mlezi wa Manispaa ya Ilemela

**Mungu anasamehe, Mazingira hayasamehi Tunza Mazingira yakutunze.**



Mh. Dkt. Angeline S.L Mabula (Mb)
Naibu Waziri Wa Ardhi

"Uwe hodari tu na ushujaa mwingi, uangalie kutenda sawasawa na sheria yote aliyokuamuru Musa mtumishi wangu; usiiache, kwenda mkono wa kuume, au wa kushoto, upate kufanikiwa sana kila uendako".
Yoshua 1:7